tigo pesa SportPesa
MAOKOTO Deilee!
WEKA ZAIDI, BET USHINDE ZAIDI
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



## CLEOPA MSUYA: Tuna la kujifunza toka CHADEMA

UKURASA 11




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatano Septemba 6, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581425

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## Wahamiaji wasiohamishika wapewa uraia Zanzibar

UKURASA 2

### MKUTANO MIFUMO YA CHAKULA

# Tanzania yanadi chakula chake



**MAFUTA** ya kula, sukari, muhogo vyawekewa mkakati... *Endelea Uk. 3, 5 & 7*




Rais Samia Suluhu Hassan akihutubia wakuu wa nchi mbalimbali, taasisi na mashirika ya kimataifa katika Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi barani Afrika 2023, jijini Nairobi, Kenya jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 2

### MCHENGERWA, SILAA WATEMA CHECHE

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amesema asilimia 45 ya wakuu wa wilaya wamebainika kuwa hawatekelezi...

UKURASA WA 3

### DC KIKAANGONI KATIKA BARAZA LA MAADILI

MKUU wa Wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro, Dk. Julius Ningu, amefikishwa katika Baraza la Maadili kwa tuhuma za kutoa lugha za matusi, vitisho na kuwaweka mahabusu watumishi wa umma...

UKURASA WA 19

### KESI YA MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

REVOCATUS Muyela, mshtakiwa wa pili katika kesi ya mauaji ya Aneth Msuya, amemtaka Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Arusha, SSP David Mhanaya, kuacha kumchafua kwa kumwita...



### TISHIO EL-NINO

## WAKAZI MABONDENI WASEMA WAKO TAYARI KUHAMA, SHIDA NI PA KWENDA

UKURASA 4

Sehemu ya nyumba zilizojengwa katika bonde la Mto Msimbazi, Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam, ambazo wakazi wake hulazimika kuzikimbia kutokana na mafuriko nyakati za mvua. **PICHA: JENNIFER GILLA**

**MICHEZO** MIQUISSONE AHAIDIWA USHINDI SIMBA, AL AHLY UK. 24

**KATUNI** UK. 6




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (kulia), akizungumza katika mkutano wa kimataifa wa mifumo ya chakula Afrika uliojumuisha wadau mbalimbali wa sekta ya chakula ndani na nje ya bara la Afrika. Kushoto ni Mkuu wa Idara ya Mikakati wa Benki ya Rabobank, Ben Valk na Makamu wa Rais wa Shirika la Farmer Solution Africa, Mehdi Filali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahamiaji wasiohamishika wapatiwa uraia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, jana alikabidhi vyeti vya uraia kwa kundi la wahamiaji 3,319 wasiohamishika katika hafla iliyofanyika katika viwanja vya Ikulu, Zanzibar.

Akizungumza baada ya kukabidhi vyeti hivyo, Dk. Mwinyi alitaka Idara ya Uhamiaji ambayo ndiyo yenye dhamana ya masuala ya uhamiaji nchini, kuendelea kuziimarisha sheria zilizopo hususan sheria ya uraia wa Tanzania.

Alisema hivi sasa mataifa mbalimbali duniani yanaendelea kuimarisha sheria zao za uhamiaji na uraia kwa lengo la kudhibiti uingiaji, ukaaji na utokaji wa watu ili kulinda mipaka na kuhakikisha amani na usalama vinaimarika katika mataifa yao.

“Sheria hii haijafanyiwa mapitio kwa kipindi kirefu. Huu ni wakati mwafaka wa kuiangalia upya kwa madhumuni ya kuiwezesha kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazowahusu wananchi na wageni wanaofika hapa nchini,” alisema.

Alisema Zanzibar inaandika historia mpya ya kulikamilisha jambo hilo kubwa la kuwapa uraia ndugu zao ambao wameishi nao kwa zaidi ya miaka 50 sasa wakiwa na asili ya mataifa jirani ya Burundi, Comoro, Msumbiji na Rwanda.

“Nachukua nafasi hii kuwapongeza sana ndugu zetu hawa kwa kupata hadhi hii ya kutambuliwa kuwa raia wa Tanzania ikiwa ni baada ya kukamilisha matakwa ya kisheria kwa mujibu wa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,” alisema.

Dk. Mwinyi pia alisema serikali zote mbili za Muungano na ile ya Zanzibar zimefurahia kuona kuwa hatimaye suala hilo limekamilika kama alivyotoa ahadi baada ya kuingia madarakani mwaka 2020.

“Leo (jana) napata faraja kuona kuwa dhamira njema ya Serikali na ndoto ya muda mrefu waliyokuwa nayo ndugu zetu hawa, imetimia. Kumalizika kwa jambo hili kunawafanya tuwatambue kuwa raia wa Tanzania badala ya wahamiaji wasiohamishika,” alisema.

Dk. Mwinyi alisema ni matumaini yake kuwa waliokabidhiwa kadi hizo za uraia wataipata heshima inayostahili hadhi ya kuwa raia kwa kuwa raia wema.

“Kwa hakika ndugu zangu mna wajibu wa kuendeleza utiifu wenu wa sheria na kujiepusha na vitendo viovu ili msipotoshe dhamira njema ya Serikali ya kukupeni uraia wa Tanzania,” alisisitiza.

Aidha, aliwataka kushirikiana katika kulinda na kudumisha amani iliyopo kwa faida ya sasa na wale watakaokuja baadaye.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni Yussuf akizungumza kwenye hafla hiyo, alizipongeza serikali kwa busara za kuwasamehe Watanzania hao takribani Sh. milioni mbili za kulipia uraia wao sambamba na kufanikisha jambo hilo.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, alimpongeza Rais Mwinyi kwa kukamilisha ahadi ya kuzitatua changamoto za wahamiaji hao wasiohamishika tangu alipowaahidi mwaka 2020 kuitekeleza kwa vitendo.

Kamisha Jeneral wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala, alisema jeshi hilo lina jukumu la kuratibu masuala yote ya uhamiaji nchini yanayohusu raia wanaoomba uraia kisha kukabidhi kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Pia, alisema Idara ya Uhamiaji Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifanya utambuzi kwa Watanzania hao baada ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Watanzania hao waliokuwa wakikabiliwa na changamoto za kukosa haki zao za msingi kisheria zikiwemo hati za uraia, hati za kusafiria na haki zingine wanazopatiwa Watanzania halisi.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
05.09.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **08.09.2023** hadi **14.09.2023** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha magari matupu wenye vipimo vikubwa kutoka **Mzenga** kuelekea **Bandari ya Dar Es Salaam,** gari hilo lenye namba za usajili **NRB97300 / NRB15200 DS00TGGP / NRB43293**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita** | **36.5** |
| **Upana** | - | **Mita** | **4.30** |
| **Kimo** | - | **Mita** | **4.60** |

3. Njia itakayotumika: **Mzenga hadi Bandari ya Dar Es Salaam** kupitia **Barabara ya Morogoro, Barabara ya Mandela** gari litasafiri muda wa mchana ***( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

117586602


# Mchengerwa, Silaa watema cheche

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amesema asilimia 45 ya wakuu wa wilaya wamebainika kuwa hawatekelezi majukumu yao, hivyo kuahidi kuwa hatawafumbia macho pamoja na watumishi wasiofanya kazi na kujiona miungu watu.

Wakati Mchengerwa akibainisha hayo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, ameagiza siku 100 za kwanza akiwa ofisini, zitumike kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mchengerwa alisemahayo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza baada ya kuwasili na kukabidhiwa ofisi na mtangulizi wake, Angellah Kairuki, ambaye amehamishiwa Wizara ya Maliasili na Utalii katika mabadiliko ya Baraza la Mawaziri yaliyofanyika hivi karibuni.

Alisema amedhamiria kurejesha TAMISEMI kwa wananchi kwa kuwafikia na kusikiliza kero zao.

“Kuanzia sasa wakuu wa mikoa wote, wakuu wa wilaya washuke chini kusikiliza kero za wananchi. Asilimia 45 ya wakuu wa wilaya hawafanyi kazi kabisa, hawasikilizi kero za wananchi. Kwa hiyo tunataka kila mmoja afanye kazi ili kutimiza malengo ya Watanzania, malengo ya Chama Cha Mapinduzi na malengo ya Rais wetu.”

“Hufanyi kazi nitakuweka kando na hii ni kwa yoyote. Hakuna ‘god father’ hapa. Kama mtu ameletwa na mtu kwa jina lazima afanye kazi kwa bidii na hii ni kwa kila mtumishi. Hii si kwa watendaji wa wizara pekee bali mpaka kijijini kama umepata kazi kwa jina la mtu ufanye kazi kwa bidii sitakubali hata kidogo.

“Serikali imepeleka fedha nyingi lakini miradi mingi watu wanakula rushwa, ubadhirifu wa fedha miradi, uvivu na uzembe wengine wanafanya kampeni za siasa hawafanyi kazi walizoteuliwa nazo. Tutamshauri Mheshimiwa Rais tutawaweka kando tunataka kila moja afanyekazi kwa bidii ili tuweze kufanikiwa,” alisema.

Kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Mchengerwa aliwaonya wakurugenzi wa halmashauri ambao wamekalia fedha za miradi na kusisitiza kuwa hataongeza muda wa kukamilisha miradi hiyo.

“Waziri (Kairuki) umesema kuna miradi mingi ambayo tayari imeshaanzwa lakini kuna baadhi ya watu hawajaitimiza, uliwawekea deadline, sitaongeza hata siku moja, na nitaomba unikabidhi hayo makaratasi, kila mmoja kule aliko lazima ajue, wakurugenzi ambao wamekalia fedha za miradi sitaongeza siku hata moja,” alisema.

Mchengerwa alisema serikali imepeleka fedha nyingi za kutekeleza miradi katika mamlaka za serikali za mitaa na kubainisha kuna baadhi wasiotekeleza wajibu wao na kusisitiza kuwa hatamvumilia mtu yeyote.

Kadhalika, alisema hatakubaliana na uonevu wa watumishi na kuwataka Maofisa Utumishi katika mamlaka za serikali za mitaa kusikiliza kero za watumishi na kuzitatua.

“Najua asilimia 76 ya watumishi wa umma wako TAMISEMI hivyo tuna kazi kubwa ya kulinda haki za watumishi, nilipokuwa utumishi walinyooka, hivyo Maofisa Utumishi huko mliko nataka msikilize kero za watumishi kwenye maeneo yenu,” alisema.

**SILAA NA ARDHI**

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, ameelekeza watendaji wa sekta ya ardhi nchini kuhakikisha ndani ya siku 100 kuanzia juzi, wanatatua migogoro ya ardhi kwa kadri ya uwezo wa nafasi zao.

Pia ametaka waliovamia maeneo ya wazi kuanza kuondoka mara moja huku akielekeza viongozi na watendaji wa wizara wenye mamlaka ya kusimamia sheria kuhakikisha ndani ya muda huo maeneo hayo yanakuwa wazi.

Silaa alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na menejimenti ya wizara baada ya kukabidhiwa ofisi na mtangulizi wake, Dk. Angeline Mabula, katika ofisi za wizara hiyo Mtumba, Dodoma.

“Nawaomba na kuwaelekeza watendaji wote ambao sheria imewapa mamlaka kwa kiasi chao kutatua migogoro ndani ya siku hizi 100 kila mmoja atatue kwa kadri ya uwezo wake,” alisema.

**-Imeandikwa na Augusta Njoji na Munir Shemweta, DODOMA**

## HABARI KITAIFA

# Serikali yaja na mkakati kuboresha zao la muhogo

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imeanza mikakati ya kuboresha zao la muhogo ikiwamo kuchanganya kwenye unga wa sembe na ngano ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na kukidhi soko la dunia.

Pia, imeanza kufanya utafiti wa kupatikana mbegu ya muhogo yenye ladha moja ili kukidhi soko la kimataifa baada ya kubainika kuwa zao hilo lina ladha zinazofautiana, hivyo kupunguza mvuto katika soko la nje.

Waziri wa Kilimo, Husein Bashe, alisema hayo jana katika Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) alipokuwa anatangaza fursa za uwekezaji kwa wadau wa kilimo kutoka nchi mbalimbali.

Alisema miaka mitatu iliyopita walianza kulitangaza zao hilo kwa kutazama soko la China na kubaini matumizi yake si kwa wafanyabiashara wa nje tu bali hata wa ndani.

Kwa mujibu wa Bashe, changamoto kubwa kwa sekta ya kilimo ni tija hali inayosababisha wakulima kuzalisha mazao yasiyo na ubora wa kushindana katika masoko ya nje ya nchi.

Alisema ili mkulima azalishe kwa tija anatakiwa kupata miundombinu rafiki kama vile umwagiliaji na mbegu bora kwa kuwa changamoto ya soko, mwenendo wa dunia na ongezeko la idadi ya watu kwenye mazao ya chakula si kubwa.

Hata hivyo, alisema Tanzania bado inapitia changamoto ya bei ya chakula kupanda kwa sababu tija shambani ni ndogo ndio maana lengo la mkutano huo ni kuionesha dunia rasilimali zilizopo nchini na namna gani Watanzania washiriki kuzitumia rasilimali hizo ili kufanya biashara ya chakula ulimwenguni.

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli, alisema kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), wameshaanza kufanya utafiti ili kupata mbegu ya muhogo itakayotoa ladha moja na inayohimili athari za mabadiliko ya tabianchi ili likidhi mahitaji ya soko la dunia.

Pia alisema, alisema suala hilo linakwenda sambamba na upimaji wa afya ya udongo, ili wakulima wazalishe katika maeneo ambayo ni sahihi na kutoa zao lenye ubora utakaoshindana katika soko hilo.

Kwa Mujibu wa Mweli, utafiti huo pia utafanyika kwenye mazao ya matunda ikiwamo machungwa na mananasi ambayo yamekuwa na ladha isiyofanana hali inayorudisha nyuma mauzo yake katika soko la dunia.

**BIASHARA MAJANI**

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewataka wafugaji kujenga utamaduni wa kubiasharisha majani ili kutosheleza mifugo katika malisho na kuondosha migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Akizungumza jana wakati wa ufunguzi rasmi wa mkutano huo, jijini Dar es Salaam, Waziri Ulega alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi mifugo imekuwa ikihangaika kutafuta malisho kwa kiasi kikubwa.

Ulega alisema, kubiasharisha majani pia itasaidia mifugo wakati wa uhaba wa malisho, na kuongeza kipato kwa kufanya biashara ya kuwauzia wale ambao hawajapata mvua kwa miaka mingi na wanaohangaika kutafuta malisho kwa ajili ya mifugo yao, huku akibainisha tija ya mkutano huo katika sekta ya mifugo na uvuvi.

"Mkutano huu ni wa fursa na kuonyesha namna ambavyo nchi yetu imejaliwa kwa kiasi kikubwa sana na tunahitajika kuingiza mitaji, teknolojia, uzoefu na hatimaye tuweze ku 'unlock' fursa tulizonazo kwa faida ya taifa letu," alisema Ulega.

Aliongeza kuwa lazima wakubaliane kwamba kilimo mazao, ufugaji, na uvuvi vinategemeana na kwamba wanapozungumzia suala linalohusu uzalishaji wa mifugo wana asilimia 70 ya mahitaji yanayotokana na mazao yanayotoka kwenye kilimo.

"Ni watu ambao tunategemea wakulima, wafugaji wote ndio hao hao lakini jambo kubwa ambalo leo 'jana' tumelionyesha ni juu ya fursa pana tuliyonayo kama nchi na kwamba ni namna gani tumejipanga vyema kupokea uwekezaji, kwakuwa ukweli ni kwamba shida yetu kubwa ni mitaji, teknolojia na masoko.

"Hata sisi upande wa mifugo mambo ambayo tumeyapa kipaumbele na kesho 'leo' tutaonyesha kazi yetu na fursa zilizoko na tayari tumejipanga kwa mtu yoyote ambaye yuko tayari kuja kuwekeza wa ndani au nje kumuonyesha mahala pa kuwekeza ni wapi ili mtaji wake uweze kupatikana kwa maana ya faida," alisema Ulega.

**-Imeandikwa na Jennifer Gilla na Maulid Mmbaga**

# DC matatani akifikishwa katika Baraza la Maadili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro, Dk. Julius Ningu, amefikishwa katika Baraza la Maadili kwa tuhuma za kutoa lugha za matusi, vitisho na kuwaweka mahabusu watumishi wa umma.

Kikao cha baraza hilo kiliketi jana jijini hapa chini ya Mwenyekiti wa Baraza hilo, Jaji mstaafu Rose Teemba. Upande wa mlalamikaji uliwakilishwa na Wakili wa Serikali, Emma Gelani.

Akiwasilisha malalamiko hayo mbele ya Baraza hilo, Wakili Emma alidai kiongozi huyo alitenda kosa hilo akiwa Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma ambako alitoa lugha hizo na kuwaweka rumande baadhi ya watumishi wa umma akiwamo Mtendaji wa Kata ya Rwinga, Mario Fabian.

Ilidaiwa kuwa mlalamikiwa huyo wakati akitekeleza majukumu yake kikazi amekuwa akitumia lugha chafu na matusi kwa viongozi na watumishi wa umma alipokuwa katika ziara ya ukaguzi wa miradi mbalimbali kinyume cha kifungu cha 6(1)(a) na (b), hivyo kukiuka Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma kifungu cha 6(2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

"Mwenyekiti, kitendo hiki ni kinyume cha maelekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia barua yake ya tarehe 1/4/2019 kwenda kwa wakuu wa mikoa na wilaya kuhusu matumizi sahihi ya Sheria ya Tawala za Mikoa Sura ya 97 inayotoa utaratibu wa kumweka mtu mahabusu kwa muda wa saa 48," alidai.

Kwa mujibu wa Wakili huyo Mkuu wa Serikali, maelekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, yanamtaka Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa wilaya kutoa maelezo kwa njia ya maandishi kwa Jeshi la Polisi kabla au muda mfupi baada ya kuamuru kuwekwa ndani na kutoa sababu za msingi za kumweka mahabusu mtuhumiwa.

"Dk. Ningu hakutoa maelezo yoyote kwa Jeshi la Polisi kuhusiana na kukamatwa watumishi wa halmashauri na mafundi waliokuwa wanatekeleza mradi ya UVIKO-19 katika Wilaya ya Namtumbo kinyume cha maelekezo ya sheria," alidai.

Shahidi ambaye ni Mkuu wa Polisi wilayani humo, William Mwamafupa, alidai alitekeleza agizo la kuwaweka ndani lililotolewa na Mkuu wa Wilaya baada ya kushauriana na wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya.

"Kisheria Ofisi ya Mkuu wa Wilaya hutakiwa kuandika barua ili kutekeleza amri ya kuwaweka ndani, lakini haikufanyika hivyo," alidai.

Mlalamikiwa huyo (Dk. Ningu) alikana kutumia lugha hizo na kwamba uamuzi wa kuwaweka rumande ulitokana na ushauri wa kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya na si uamuzi wake peke yake.

Alidai amewasilisha kielelezo cha barua aliyoandika kwa Mkuu wa Polisi Wilaya, lakini imeondolewa kutokana na kutofuata taratibu za kisheria za kuwasilisha vielelezo.

Baada ya baraza hilo kusikiliza hoja zote za pande mbili, Mwenyekiti wake, alisema watakaa kujadili kwa kina na uamuzi watajulishwa kwa mujibu wa taratibu.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

**UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO LA MBARALI NA MADIWANI KATIKA KATA SITA ZA TANZANIA BARA**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote wa Jimbo la Mbarali, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Mkoani Mbeya na kata sita (6) za Tanzania Bara kuwa kutakuwa na Uchaguzi Mdogo wa Ubunge Jimbo la Mbarali na Madiwani siku ya Jumanne tarehe 19 Septemba, 2023. Kata zinazofanya Uchaguzi ni Nala (Dodoma CC), Mfaranyaki (Songea MC), Old Moshi Magharibi (Moshi DC), Marangu Kitowo (Rombo DC), Mtyangimbole, (Madaba DC) na Mwaniko (Misungwi DC).

1. SIKU: Wananchi watapiga kura siku ya Jumanne tarehe 19 Septemba, 2023
2. VITUO: Upigaji kura utafanyika katika vituo vilivyotumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020
3. MUDA: Vituo vitafunguliwa saa 1:00 kamili Asubuhi na kufungwa saa 10:00 kamili Jioni

**Mambo ya kuzingatia wakati wa Uchaguzi**

1. Mpiga Kura anatakiwa kwenda katika kituo alichojiandikisha na kadi yake ya mpiga kura siku ya uchaguzi.
2. Wapiga kura waliopoteza kadi zao za kupigia kura au zilizoharibika, wanaruhusiwa kutumia vitambulisho mbadala kimojawapo ya: -
   a) Hati ya kusafiria,
   b) Leseni ya Udereva, na
   c) Kitambulisho cha Taifa.

Majina yote matatu yaliyomo katika vitambulisho mbadala yafanane na yaliyomo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

3. Mpiga Kura akifika kituoni anatakiwa kupanga mstari.
4. Mpiga kura anatakiwa kufuata maelekezo yote atakayopewa na Karani Mwongozaji wa kituo.
5. Mpiga kura awapo kituoni anatakiwa kutoa kipaumbele kwari wapiga kura wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokuwa nao kituoni.
6. Watu wenye mahitaji maalum wanaruhusiwa kwenda kituoni na wasaidizi.
7. Ifikapo muda wa kufunga kituo saa 10:00 kamili Jioni kama wapiga kura bado wapo kwenye mstari, mlinzi wa kituo atasimama nyuma ya mtu wa mwisho na zoezi la upigaji kura litaendelea hadi wapiga kura walio kwenye mstari watakapomalizika. Mpiga kura atakayefika zaidi ya muda wa kufunga kituo hataruhusiwa kupiga kura.
8. Baada ya kumaliza kupiga kura, mpiga kura anatakiwa kuondoka eneo la kituo cha kupigia kura.

Kumbuka kupiga kura ni haki yako ya msingi jitokeze siku ya uchaguzi ukamchague Mbunge na Diwani unayemtaka siku ya Jumanne,tarehe 19 Septemba, 2023.

**Kailima, R. K.**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

217578702

## TISHIO LA EL-NINO

# Wananchi: Tuko tayari kuhama mabondeni, shida pa kwenda

**Na Jenifer Gilla**



Sehemu ya nyumba zilizojengwa katika bonde la Mto Msimbazi, jijini Dar es Salaam, ambazo wakazi wake hukumbwa na kadhia ya mafuriko wakati wa mvua. **PICHA: JENIFER GILLA**

WAKATI Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ikihadharisha ujio wa mvua ya El-Nino mwezi ujao, wakazi wanaoishi mabondeni nchini, wamesema wako tayari kuhama kwa sharti la kupewa mbadala pa kwenda.

Mwezi uliopita, TMA iliwataka wakazi wa maeneo hayo kuchukua tahadhari za athari za mvua hiyo inayotarajiwa kunyesha kati ya Oktoba na Desemba mwaka huu.

Kwa mujibu wa TMA, mvua hiyo inaweza kuleta madhara kwa binadamu na mazingira, ikiwamo vifo, mafuriko, maporomoko ya ardhi, upotevu wa mali, magonjwa ya mlipuko na uharibifu wa miundombinu.

Udadisi wa Nipashe unaoendana na kauli rasmi ya serikali kutoka vikao vya Bunge vinavyoendelea Dodoma, umepata mrejesho wa msimamo wa sehemu kubwa ya wakazi hao wa bondeni, wakionesha utayari wao kuhama, kikwazo pekee kilicho mbele yao ni mbadala wa makazi.

Pia, ni msimamo unaoendana na ushauri kwa serikali kuwezesha ujenzi wa ukuta katika kingo za Mto Msimbazi ili kuzuia usiendelee kutanuka, kubomoa nyumba na kuleta uharibifu mwingine kwa wakazi wa maeneo ya karibu.

Mkazi wa Mtaa wa Msimbazi, Kata ya Msimbazi, Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam, Shomari Omari, anasema yuko tayari kuondoka eneo hilo na kwenda kuishi kokote ambako serikali itampatia eneo kwa kuwa familia yake inateseka kila mvua inaponyesha.

Anasema kuwa wakati anahamia eneo hilo mwaka 1984, kulikuwa na mto mdogo uliokuwa unatiririsha maji safi yaliyokuwa yanatumika nyumbani, lakini kadiri mvua ilivyokuwa inavyesha, mto ulizidi kutanuka huku shughuli za binadamu zikichochea uharibifu.

"Watu wanavyochimba mchanga kwa ajili ya ujenzi, wanaongeza kutanua huu mto. Matokeo yake, mvua ikinyesha inasababisha mmomonyoko wa udongo na kama kuna nyumba karibu zinabomolewa. Nimeshuhudia nyumba nyingi zimebomolea na kuwaacha watu bila makazi," alisema.

Mkazi mwingine wa mtaa huo, Mary Charles, anasema anaishi na familia katika eneo hilo kwa shaka kutokana na hofu kwamba kuna siku mvua inaweza kusababisha vifo, lakini hawana sehemu nyingine ya kwenda kutokana na hali ya kipato chao, ni kidogo.

Mama huyo anayefanya biashara ya kuuza mboga, anasimulia madhara wanayokutana nayo mvua inaponyesha, yanajumuisha maji kuingia ndani na kuharibu mali zao, ikiwamo kulowesha magodoro, viti na tope kujaa ndani. Hulazimika kutumia gharama kubwa kufanya ukarabati na usafi.

Anasema mafuriko hayo pia yanasababisha maradhi kwao ikiwamo mafua, kuumwa vifua na kuhara. Wakati mwingine hulazimika kwenda kupata hifadhi katika shule iliyoko karibu na eneo hilo.

"Kuna wanaokwenda kujihifadhi kwa ndugu zao, lakini sisi tusio na ndugu karibu tunakwenda kujihifadhi kwenye shule ya msingi iliyopo karibu mpaka majanga yatakapoisha. Kwa kweli tunaishi kwa shida, tunaomba serikali itushike mkono," anasema kwa uchungu Mary.

Zeofania Damas, anasema kuwa mafuriko ya mara kwa mara yameshusha thamani ya eneo hilo huku akitoa mfano wa vyumba vya kupangisha havizidi Sh. 30,000 wakati maeneo mengine vyumba kama hivyo vinapangishwa kwa Sh. 50,000.

"Mimi mwenye nyumba za kupangisha, nina hasara kubwa, vyumba vyangu hapa sipangishi zaidi ya Sh. 30,000 na hata watu wanaopanga ni vijana wale 'wasela', mtu na familia yake hawezi kuja huku, kwa sababu hawezi kuvumilia nyumba ambayo mvua ikinyesha maji yanaingia ndani," alisema.

Mkazi wa Mtaa wa Kawawa, Kinondoni Mkwajuni, Manispaa ya Kinondoni, Ramla Rashid, anasema kuwa tangu ahamie huko mwaka 2020, maisha yake yamekuwa ya kuhama kila mvua inaponyesha kwa kuwa maji yanaingia ndani na kuleta madhara ikiwamo magonjwa, hasa kuhara.

"Maji yanayoingia ndani ni machafu na humu nina watoto wadogo. Kwa hiyo, wanavyoyakanyaga na kuyachezea, wanapata maradhi ya kuhara, minyoo na wakati mwingine nimonia," anasema.

Anabainisha kuwa yeye mumewe waliondoka eneo hilo mwaka 2015 na kwenda kupanga Buguruni wilayani Ilala baada ya TMA kutangaza ujio wa mvua kubwa kipindi hicho, lakini wamelazimika kurudi katika makazi yao ya awali kutokana na hali ya maisha kuwa ngumu na kukosa fedha za kuendelea kulipia kodi ya pango.

Havinitishi Juma, jirani na mama huyo, anaiomba serikali kujenga ukuta mrefu katika mto huo ili kuzuia maji kuingia katika makazi ya watu pindi mvua kubwa inaponyesha.

Mkazi wa Mtaa wa Mayoka, Kigogo Dampo, wilayani Kinondoni, Saidi Abdallah, anasema mvua inaponyesha wanapata hasara kutokana na vifaa vya umeme kama vile mafriji, redio na runinga kuharibiwa.

"Maji yanaingia na kutokea dirishani. Haya ndiyo maisha yetu, tumeshazoea. Ninatamani kuondoka, lakini nitakwenda wapi sina uwezo? Nyumba hii ni ya urithi, wakati tunahamia hapa mto ulikuwa mdogo na tunauona kwa mbali, lakini sasa hivi umetanuka hadi karibu na nyumba," alisema.

### MAMLAKA ZILIVYOJIPANGA

Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Msimbazi, Mohammed Salum, alisema wamesikia taarifa za TMA kuhusu ujio wa mvua ya El-Nino. Wanajipanga kutoa taarifa katika mtaa wake ili wananchi wachukue tahadhari mapema.

"Huwa tunatoa taarifa kupitia hafla kama vile misiba, harusi, kwa kuwa ndio sehemu pekee ya kupata kundi kubwa.

"Pia, tunapita nyumba kwa nyumba nyakati za usiku familia zinapokuwa zimerudi nyumbani, lengo ni kuhakikisha hakuna familia itakayopata madhara ya mafuriko," anasema.

Mjumbe wa shina namba moja katika mtaa huo, Frida Satu, alisema alishakaa kikao na wakazi wa eneo lake. Wamweleza wamechoshwa na hali hiyo. Serikali ikiwapa eneo, wako tayari kuondoka.

Anasema katika eneo kale, kuna kaya 64 zilizo eneo hatarishi. Mvua ikinyesha maji huingia ndani na kusababisha madhara makubwa ikiwamo vifo na uharibifu wa mali.

### SERIKALI ILIVYOJIPANGA

Ibara ya 8 ya Katiba ya nchi, inaelekeza lengo kuu la serikali ni kuhakikisha kunakuwa na ustawi wa wananchi. Je, serikali imechukua hatua zipi kuhusu tahadhari hiyo ya TMA?

August 31 mwaka huu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, alisema serikali imezielekeza kamati za usimamizi wa maafa na sekta, kushirikiana na umma kuchukua hatua kukabiliana na madhara yanayoweza kutokea wakati wa El-Nino.

Waziri huyo alitaja hatua hizo kuwa ni kutambua maeneo hatarishi na yenye viashiria vya kuathirika na maafa na kuandaa mipango ya kuzuia madhara na kukabiliana na maafa endapo yatatokea pamoja na kuainisha na kuandaa rasilimali za usimamizi wa maafa kwa kila sekta kushiriki kikamilifu katika eneo lake.

"Tunazielekeza kamati hizo zisisubiri maafa yatokee. Waanze kutambua maeneo yote hatarishi na yenye viashiria vya kuathirika na maafa na kuanza kuandaa mipango ya kuzuia madhara yoyote yanayoweza kutoka na utabiri huo wa TMA," aliagiza waziri huyo.

Waziri Jenista pia alitoa rai kwa wananchi wanaoishi na kuendesha shughuli za kiuchumi maeneo ya uwanda wa chini na pembezoni mwa mabonde ya maji, wachukue tahadhari kuchukua hatua ili kunusuru maisha na mali zao.

Kukiwa na hadhari hiyo serikalini, jana Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Stella Ikupa, alihoji bungeji mkakati wa serikali kukabiliana na athari za mvua ya El - Nino inayotarajiwa kunyesha kuanzia mwezi ujao.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Khamis Hamza Khamis, alitoa tahadhari kwa wananchi kuacha kujenga na kufanya shughuli za kijamii katika maeneo ya mabondeni ili kuepuka athari za mafuriko zinazoweza kutokea na kusababisha madhara.

"Serikali katika kipindi hiki tunawapa elimu wasijenge katika maeneo ambayo yana maji. Na wenye makazi katika maeneo hayo kwa sasa, basi waondoke ili mvua itakaponyesha wasipate madhara," alisema.

HABARI KITAIFA

# Ahukumiwa maisha jela kwa kulawiti wanafunzi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora, imemhukumu Daudi Masanja (28), mkazi wa Kata ya Igunga mjini, kifungo cha maisha jela baada ya kukutwa na hatia ya kulawiti wanafunzi wawili.

Adhabu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mfawadhi wa Wilaya ya Igunga, Lydia Ilunda.

Akitoa adhabu hiyo, alisema mshtakiwa alitiwa hatiani kwa makosa mawili ya wanafunzi, mmoja mwenye umri wa miaka 13 na wa pili ana miaka minane kwa siku moja. Alisema hukumu hiyo iwe fundisho kwa watu wenye nia ovu ili kukomesha vitendo vya kuwadhalilisha watoto wadogo na wanafunzi.

Mwendesha mashtaka wa serikali wilayani Igunga, Grace Lwila, alidai mshtakiwa alitenda makosa yote Mei 16, mwaka huu, majira ya mchana mtaa na Kata ya Igunga mjini, wanafunzi hao wakiwa wanatoka shuleni.

"Alianza kwa kutenda ukatili huo kwa mwanafunzi mwenye umri wa miaka 13 anayesoma darasa la sita kisha kwenda kwa mwanafunzi mwingine wa miaka minane anayesoma darasa la tatu kwa kuwalawiti na kuwasababishia maumivu makali," alidai.

Aliendelea kudai kuwa mshtakiwa huyo alitenda makosa hayo kinyume na kifungu cha sheria namba 154 'a' cha kanuni ya adhabu sura ya 16 mapitio ya mwaka 2022 inayozuia kutenda makosa kama hayo.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, mshtakiwa alikana na upande wa Jamhuri ulipeleka mashahidi wanane wakiwamo wanafunzi hao pamoja na daktari ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushahidi wao na kumtambua mshtakiwa na kuthibitisha kwa vielelezo vya vipimo.

Kabla ya adhabu, mwendesha mashtaka wa serikali aliomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa kwa kuwa kitendo alichofanya ni cha aibu na kimeleta fedheha kwa jamii na taifa kwa ujumla.

## Mpango ataka Afrika kuelekeza upendeleo wakulima wadogo

**Na Renatha Msungu**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amefungua Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) 2023, jijini Dar es Salaam, akihimiza nchi za Afrika kuelekeza upendeleo kwa wakulima wadogo, hasa vijana na wanawake.

Dk. Mpango ambaye pia ni mchumi, amezihimiza serikali za Afrika kuchukua hatua kuwapa wakulima wadogo pembejeo za bei nafuu, maarifa, ujuzi na fedha ili kuongeza tija katika minyororo ya thamani ya chakula.

Alitoa kauli hiyo jana katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), huku Serikali ya Tanzania ikiwa imeshapiga hatua katika eneo hilo, ikiwamo nyongeza ya bajeti katika sekta ya kilimo zaidi ya asilimia 320 katika miaka miwili iliyopita.

Dk. Mpango alitumia nafasi hiyo kueleza serikali za Afrika zinahitaji pia kuongeza uwezeshaji wa kidijitali na ufadhili wa utafiti wa kisayansi.

Alisema ni lazima wathamini kuwa vijana wao na wanawake ni muhimu kwa mifumo yao ya chakula na wanahitaji kutumia idadi yao inayoongezeka na kuhakikisha wananufaika kutokana na jasho na ubunifu wao.

"Tunapaswa kujitahidi kufanya kilimo kivutie kizazi kipya kwa kutumia teknolojia ya kisasa, upatikanaji rahisi wa ardhi, mitaji ya kuanzia na masoko yanayolenga shughuli kama vile kilimo cha bustani ambacho kinalipa haraka kiasi.

"Kuna haja ya kukomesha vitendo vya unyonyaji kwa wakulima kwa kutekeleza matumizi ya mizani na vipimo vya kawaida pamoja na kupiga marufuku mbinu za soko la mbele ili kuwalinda wakulima.

"Tanzania tumefanikiwa kuondokana na utovu wa nidhamu katika minyororo kadhaa ya thamani kama vile nyama, mchele na maharagwe, lakini bado tunahitaji kuisambaza kwenye mazao mengine ya kilimo.

"Kwahiyo, ninaziomba nchi za Kiafrika kuheshimu mipango ya biashara ya kikanda, husuan Mkataba wa Eneo Huria la Biashara ya Bara la Afrika (AfCFTA), kwa kuzingatia itifaki za kibiashara na kuondoa vikwazo visivyo vya ushuru (NTBs).

"Ukuaji wa sekta yetu ya kibinafsi na mafanikio yake katika soko la kikanda na kimataifa hutegemea jinsi sera zetu zinavyounga mkono. Hatimaye, amani na usalama ni mahitaji muhimu ya awali kwa mifumo ya chakula inayofanya kazi," alisema.

Kiongozi huyo pia alishukuru Sekretarieti ya AGRF na washirika wao kwa kutupatia fursa nyingine na kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kufanikisha mkutano huo.

"Mahudhurio ni ya kuvutia sana, na inakadiriwa idadi ya zaidi ya 3,000 kutoka zaidi ya nchi 70. Maudhui ya Mkutano huo yanaonekana kuwa thabiti, huku programu ikijumuisha wazungumzaji na watendaji mashuhuri zaidi ya 350 kuhusu masuala mbalimbali ya mada kuhusu mifumo ya chakula kikanda na kimataifa.

"Pamoja na migogoro mingi ya kimataifa ya upotevu wa bayonuai, mabadiliko ya hali ya hewa na kuenea kwa jangwa, janga la COVID-19 na vita vinavyoendelea vya Urusi na Ukraine, haki ya chakula imenyimwa kwa takriban robo ya wakazi wa Afrika," alisema.

Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi Zanzibar, Suleiman Masoud Makame, alisema kuna haja kuungana dhidi ya madhara yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi kwa kuongeza uzalishaji na kukuza ujuzi wa mifumo ya chakula.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utendaji kazi Jeshi la Polisi uendane na mfumo kidijitali

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, alifungua Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Maofisa Wakuu Waandamizi wa Jeshi la Polisi uliofanyika Oysterbay, Dar es Salaam. Katika mkutano huo, Rais aliagiza mambo kadhaa kuhusu utendaji wa jeshi hilo yakiwamo kutenda haki na kujiandaa kwa uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwakani.

Pia alisisitiza jeshi hilo kujisafisha na vitendo vya rushwa na kubambikia watu kesi kama ambavyo wananchi wamekuwa wakilalamika kiutokana na baadhi ya askari na maofisa kutuhumiwa kufanya mambo hayo.

Sambamba na hayo, Rais alieleza kukerwa na baadhi ya askari na maofisa kuwa na vitambi ambavyo vinawaondolea utimamu wa mwili katika utendaji wa kazi zao. Katika hilo, alimwagiza Mkuu wa Jeshi hilo, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, kuhakikisha askari na maofisa hao wanakuwa na mwonekano wa miili ya wastani ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo muda wowote na mazingira yoyote.

Aliyoyazungumza Rais Samia katika mkutano huo ni kama marudio kwa yale aliyoagiza katika mikutano iliyopita tangu alipoingia madarakani isipokuwa suala la vitambi. Suala la malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu ubambikiaji wa kesi amekuwa akilizungumza kila wakati na umekuwa kama wimbo uliozoeleka kama ilivyo kwa vitendo vya rushwa.

Suala la baadhi ya askari polisi limekuwa likitendeka kutokana na kujenga mazingira ya kujipatia chochote ambalo halina tofauti na rushwa. Pia rushwa ndani ya jeshi hilo imekuwa kama donda ndugu kwa kuwa liko wazi na hata wananchi wanatambua kuwa kuingia polisi ni bure lakini kutoka lazima utoe pesa.

Rushwa pia imekuwa ikitajwa ndani ya jeshi hilo hasa kwa askari wa usalama barabarani. Baadhi ya askari wamekuwa wakiwataka madereva kutoa fedha ili wawaachie pindi wanapowakamata baada ya kuvunja sheria za usalama barabarani.

Ni jambo la kufurahisha kuona kwamba serikali imeamua kuyavalia njuga masuala hayo ambayo yanaichafua taasisi hiyo iliyopewa dhamana ya kulinda usalama wa rai na mali zao. Rais ameweka bayana kwamba rushwa kwa makosa ya usalama barabarani itapungua kutokana na kuwapo mpango wa kufunga kamera mbalimbali ambazo zitawanasa wale wanaokiuka sheria.

Kuna msemo kwamba ukiona mzazi anarudia maneno yale yale kwa mtoto wake ujue kuna shida. Vivyo hivyo, Rais Samia tangu aingie madarakani, amekuwa akikemea vitendo vya rushwa na ubambikaji kesi dhidi ya raia vinavyofanywa na baadhi ya askari na maofisa wa polisi. Kwa ujumla, mambo haya yamekuwa kama kero sugu ndani ya Jeshi la Polisi, hivyo ni wakati mwafaka sasa askari na maofisa ambao wamekuwa wakijihusisha na vitendo hivyo, kubadilika mara moja na kutekeleza majukumu yao kwa kufuata sheria, taratibu na miongozo iliyowekwa. Ifike mahali kwamba wahusika watambue kwamba mambo hayo ni kama wimbo ambao umekuwa ukiimbwa na sasa unachosha.

Kubwa zaidi, ni vyema sasa Jeshi la Polisi likatambua kwamba hivi sasa dunia iko katika mabadiliko makubwa ya sayansi na teknolojia, hivyo linatakiwa kutoka katika mfumo wa analogia uliozoeleka kwa baadhi ya askari na kwenda katika dunia ya sasa ya kidigitali.

Rais alisema katika utendaji kazi ndani ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), hakuna haja ya kuwa na askari wengi wa usalama barabarani kwa sababu zinaweza kufungwa kamera katika maeneo kadhaa. Kamera hizo zitang'amua wanaokiuka sheria. Kwa mantiki hiyo, rushwa barabarani zitapungua, serikali itakusanya fedha za kutosha kutokana na faini kwa sababu ya teknolojia na askari walioko sasa barabarani watapelekwa kufanya kazi zingine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ulevi, simu safarini ni tatizo

Na Tuntule Swebe

**BARABARANI** iwe mijini au kijijini zama hizi si mahala salama. Ni kutokana na ajali za vyombo vya moto hali inayotishia maisha, kuongeza vifo, ulemavu na hata watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Ni baada ya kufiwa na walezi au wazazi , wengine wanakuwa yatima kwa sababu familia nzima inaweza kupoteza maisha kwenye ajali barabarani .

Polisi na wadau mara nyingi wanazungumzia visababishi ajali mfano, kufanya kazi muda mrefu bila kupumzika, lakini kuendesha magari yenye hitilafu ambayo hayafanyiwi, ukaguzi, matengenezo au ukarabati.

Mambo hayaiishi hapo kwani kuna baadhi ya madereva huendesha magari wakiwa hawajitambui kutokana na ulevi tena wakidaiwa kuhifadhi pombe kwenye chupa za maji.

Kukosekana sheria ya kudhibiti matumizi ya simu barabarani nalo ni tatizo wapo madereva wengine huendesha wakiwa wanachati, kusikiliza muziki wakiweka foni masikioni zenye muziki mkubwa .

Ikumbukwe huwezi kutumikia mabwana wawili kuongea na simu na kuwa makini kwenye usukuni kuna wakati utakosea mwelekeo kwani ni lazima unavutika na kuwa makini na simu na kusahau jukumu la kuendesha kwa umakini.

Si hayo tu wapo wengine huacha barabara zao na kuvamia za wanaotembea na hali hiyo husababisha vifo na majeruhi kwa wanafunzi, wazee, wenye mizigo na hata wagonjwa wanaotumia njia hizo.

Kinachowapeleka maeneo hayo ni kuwa na haraka na kuendesha magari kwa mwendokasi , wengine wakikwepa foleni , kukimbia mkono wa sheria lakini pia kujificha kutokana na mienendo ya kihalifu ambayo madereva wanaifahamu ikiwamo kubeba magendo na bidhaa haramu.

Magari ya abiria huvamia njia za wanaotembea ili kukwepa malori , madereva wakiamini kuwa magari ya mizigo, hayana mwendo na kusababisha wachelewe kuwahisha na kuwawahi abiria vituoni.

Kulala nako ni changamoto, wapo wanaoendesha magari huku wakiwa wanasinzia, kupiga miayu muda wote, na wengine wakishikilia usukani na mkono mmoja.

Ukweli ni kwamba ugumu wa maisha huwalazimisha watu kufanya kazi katika hali yoyote ili wapate riziki lakini kuendesha gari ukiwa unasinzia ni hatari utasababisha ajali inayoweza kukuua na unaowaendesha na majirani wengine wanaotumia barabara.

Uzembe huo uwe wa kulala, kufungulia muziki mkubwa, kulewa na hata kuvamia njia na madaraja ya wanaotembea si kwa madereva wa daladala pekee hata wa pikipiki na bajaji.

Licha ya kuwa usafiri wa haraka, pikipiki na bajaji zimejaa matatizo, hutumia mwendokasi mno, hupenya hata kwenye taa au chini ya magari mengine hali hii hupelekea ajali kwa wanaovuka barabara, waliosimama na hata abiria waliobebwa.

Licha ya kuwapo sheria, umakini wa kazi na ukaguzi wa vyombo ni muhimu. Ni vyema kuweka mabango ya kukataza baadhi ya tabia kama vile kuongea na simu.

Kwa mfano kuna vibao vya kuelekeza kasi au spidi iwe kilometa 50 vinaweza kuongezwa ukubwa na vikaandikwa usiongee na simu unapoendesha au weka gari pembeni uzungumza na simu.

Kadhalika, kuwepo na ukaguzi wa pumzi kutambua wanaotumia vilevi . Kadhalika ukaguzi ufanywe na mamlaka za kusimamia usafiri barabarani wakiwamo maofisa wa LATRA kwa kushirikiana na wataalamu wakiwamo polisi na wahandisi magari.

Ni vyema pia kusimamia suala la pikipiki kubeba abiria wengi mfano mshikaki kwenye pikipiki , kupakiza watu wengi kwenye bajaji wakikaa hadi kwenye kiti cha dereva.

Kufuatilia leseni liwe jambo la kila wakati kwa sababu wapo madereva waliojifunza kuendesha pikipiki , bajaji hata magari nyumbani na vijiweni wote hao wakiwa chanzo cha ajali.

Madereva wasio na leseni huzuka na kuendesha usiku tena wengine wakibeba mchanga, kokoto na vifusi na hao pia huwa mwanzo wa ajali na misiba wasimamizi wa sheria wasilale wahakikishe hilo nalo linafuatiliwa na sheria ichukue mkondo maana tusipoziba ufa tutajenga ukuta.

## MKUTANO MIFUMO YA CHAKULA AFRIKA

# Bashe aipa mbinu Afrika kukabili umaskini

**Na Renatha Msungu**

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema Bara la Afrika linapaswa kuukabili umaskini kwa kuongeza idadi ya vijana na wanawake katika ushiriki wa kilimo cha uzalishaji wenye tija na utakaoleta matokeo chanya.

Bashe alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Kilimo Biashara uliofanyika jijini Dar es salaam, ukilenga kujadili mazao ya kilimo, hususani kunde na mbegu za mafuta pamoja na mpango wa kuhifadhi mbolea na mbegu.

Waziri Bashe alisema Tanzania iko tayari kuwa kapu la chakula barani Afrika na sehemu nyingine duniani, ndio maana serikali inaweka mikakati kuwekeza katika kilimo na kuisimamia vizuri sekta hiyo.

"Imefika wakati wa nchi yetu kuwa kapu la chakula, ambalo lina uwezo wa kulisha maeneo mbalimbali barani Afrika na kwingineko duniani," alisema Bashe.

Alisema washiriki wanapaswa kujikita katika mijadala ya kuona ni namna gani Tanzania inaweza kutosheleza mahitaji ya ndani ya chakula na kuuza nje ya nchi kwa kuzingatia misingi ambayo inakiweka kilimo katika biashara.

Alifafanua zaidi ya kuwa kilimo kikitumiwa vizuri kinaweza kubadilisha jamii kuwa na biashara ya uhakika, lakini hilo litawezekana kwa kutatua changamoto mbalimbali zilizopo ndani ya sekta hiyo.

Bashe aliwataka wakulima na wafanyabiashara wadogo kutumia Mkutano wa Mifumo ya Chakula Afrika ulioanza jana jijini Dar es Salaam kama fursa ya kupanua wigo wa kujiendeleza katika kilimo biashara.

Kwa kutambua fursa hiyo muhimu, Waziri Bashe aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kushiriki katika mkutano huo ambao utaleta manufaa kwa jamii na taifa kutokana na mambo mbalimbali ambayo yatajadiliwa na washiriki kutoka nchi mbalimbali barani Afrika.

Alisema ni lazima kilimo kipewe kipaumbele kikubwa hasa kwa kizazi cha sasa kwa kuwa ni taifa la kesho na wanapaswa kujua kilimo kina manufaa makubwa kikifanywa kwa kuzingatia kanuni za kilimo zinazosimamiwa na wataalamu.

Mkutano wa Mifumo ya Chakula ulianza jana katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam, kukiwa na washiriki zaidi ya 3,000 toka nchi mbalimbali.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akibonyeza kitufe kufungua Mkutano wa Jukwaa la Chakula Afrika (AGRF) jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Rais wa AGRF, Dk. Agnes Kalibata. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wafugaji samaki wapongeza serikali mazingira ya biashara

**Na Maulid Mmbaga**

WAFUGAJI wa samaki wamesema mikakati na kipaumbele kinachotolewa na serikali katika sekta hiyo kimewasaidia kuongeza tija na mnyororo wa thamani.

Juzi, baadhi ya washiriki wa Mkutano wa Jukwaa la Chakula Afrika (AGRF) ulioanza jana hadi Ijumaa, walitembelea miradi mbalimbali ya ufugaji ikiwa ni pamoja na Shamba la Ufugaji Samaki la TANLAPIA lililoko Bagamoyo, mkoani Pwani, kwa ajili ya kujifunza fursa za uwekezaji.

Katika ziara hiyo, Mkurugenzi wa Kampuni ya TANLAPIA, Baraka Kalangahe, alisema ujenzi wa mradi huo ulianza mwaka 2020 na mpaka sasa wameshaanza uzalishaji ambao umefikia tani 30 za samaki kwa mwezi ambazo wanaziuza nchini.

Alisema sekta ya ufugaji ina fursa nyingi nchini, akieleza kuwa wao wamewekeza, lakini nafasi bado ipo kubwa. Wanaendelea kuongeza jitihada ili wafikie uzalishaji wa zaidi ya tani 10,000 kwa mwaka, akisisitiza wadau hao kuzitumia fursa zilizopo kwa kufanya uwekezaji.

"Tunashukuru kwa kutembelewa na ugeni huu kwa sababu ni wa tofauti. Pia, tunaishukuru serikali kwa kutupa fursa hii adhimu ambayo nina imani italeta manufaa makubwa kwetu kama wafugaji na Taifa kwa ujumla".

"Tunaendelea kushukuru serikali kwa sababu bila msaada wao, tusingeweza kufika hapa tulipo. Hii ina maana kubwa kwetu kwa sababu inaifanya sekta ya ufugaji na uvuvi izidi kukua na kuleta tija kwa Watanzania na Taifa kwa ujumla wake," alisema.

Kalangahe alibainisha kuwa licha ya mafanikio hayo, wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji chakula cha samani nchini, alibainisha kuwa kwa siku wanatumia tani moja. Kwa kiasi kikubwa wanaagiza nje. Hakifiki kwa wakati na kuwafanya watumie gharama kubwa.

"Kama serikali ikitaka hii sekta ikue kwa haraka tuliangalie hili suala kwa mapana na marefu zaidi, iweke mazingira mazuri ya kuwafanya watu wakapenda kuwekeza katika uzalishaji wa chakula kwa sababu uhitaji ni mkubwa".

"Inawezekana mwekezaji katika eneo la chakula akaona hofu kwamba wanunuzi wapo? Soko lipo kwa sababu sisi hapa wakati mwingine mahitaji yanaongezeka, tunatumia hadi zaidi ya tani moja na nusu kwa siku, hivyo ukijumlisha sisi na wengine wadogo mahitaji yanakuwa makubwa mno," alisema Kalangahe.

Alisisitiza serikali iliangalie suala hilo ili kuhakikisha wanaondoa vitu ambavyo vinaweza kusababisha baadhi ya jitihada kukwama.

Alisema upatikanaji chakula cha samaki ukiongezeka, sekta hiyo pia itapiga hatua kwa kiasi kikubwa.

Agata Chua, Mfugaji wa Samaki na Mkazi wa Kigamboni, ambaye ni miongozi mwa waliopata fursa ya kutembelea mradi huo mkubwa wa TANLAPIA, alisema amejifunza teknolojia nyingi ambazo zimemwongeza uelewa katika ufugaji, ikiwamo ya kuongeza hewa ya Oksijeni kwenye maji, kitu ambacho hakukijua awali.

# Waziri aonesha fursa mafuta ya kula, sukari

**Na Restuta James**

WAZIRI wa Uwekezaji na Mipango amesema wawekezaji wanapaswa kuangalia fursa iliyopo katika mafuta ya kula na sukari kwa kuwa ni eneo lenye uwezo wa kurudisha haraka mtaji kutokana na soko lake kuwa kubwa.

Prof. Kitila Mkumbo aliyasema hayo jana katika Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) unaoendelea jijini Dar es Salaam, ukikutanisha wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi.

"Katika nchi nyingi za Afrika, ikiwamo Tanzania, mafuta ya kula na sukari ni miongoni mwa bidhaa tano zinazoagizwa zaidi kutoka nje, wakati huohuo malighafi za kilimo ni miongoni mwa bidhaa ambazo Tanzania inauza zaidi nje," alisema.

Waziri huyo alisema huo ni ushahidi kwamba mtu akiwekeza katika kilimo na mnyororo wa kuongeza thamani bidhaa za sekta hiyo, atarudisha mtaji wake ndani ya muda mfupi.

"Usalama mdogo wa chakula ni changamoto ya kidunia inayohitaji ufumbuzi wa pamoja kama yalivyo mabadiliko ya tabianchi. Afrika iko kwenye nafasi ya pekee ya kukabili janga hili la kidunia kutokana na kwamba ina ardhi ya kutosha kuzalisha chakula," alisema. Prof. Mkumbo alisema jukwaa la AGRF linapaswa kutoa mbinu za kukabili changamoto hiyo ili kuihakikishia dunia usalama wa chakula.

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Emmanuel Tutuba, alisema wataendelea kusimamia sekta ya fedha ili kuimarisha kilimo kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wakulima na wawekezaji walioko katika mnyororo wa kuongeza thamani.

"Ni asilimia 44 tu ya ardhi ya Tanzania yenye rutuba inayotumika kwa kilimo, ni wakati mwafaka sasa kutumia ardhi hii kuzalisha chakula cha kutosha," alisema.

Gavana Tutuba alisema BoT imeshusha riba ya benki hadi asilimia sita ili kuwawezesha wakulima na wadau wa kilimo kupata mkopo kwa riba ya asilimia tisa.

Makamu Mkurugenzi wa Bodi ya Maendeleo Rwanda, Nelly Mkazayire, alisema sekta ya kilimo nchini mwake imepewa mazingira wezeshi. Anayetaka kuwekeza Rwanda anaweza kupata vibali vyote ndani ya saa nane.

"Vibali vinapatikana ndani ya eneo moja na tumetengeneza mazingira mazuri ya uwekezaji ikiwamo misamaha ya kodi, upatikanaji mikopo na muda wa urejeshaji... Hili limetusaidia kuvutia uwekezaji ambao utaimarisha mfumo wa chakula," alisema.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

## *KUMB: PPR/2023 - 09/01*

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 6 SEPTEMBA 2023

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini zitakazotumika kuanzia Jumatano, **tarehe 6 Septemba 2023 saa 6:01 usiku.** Kwa mwezi Septemba 2023, bei za rejareja za mafuta katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ni kama ifuatavyo:

| Mkoa | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| | TZS/Lita | | |
| Dar es Salaam | 3,213 | 3,259 | 2,943 |
| Tanga | 3,259 | 3,305 | 2,989 |
| Mtwara | 3,285 | 3,332 | 3,016 |

Mabadiliko ya bei za mafuta kwa mwezi Septemba 2023 yanatokana na **kupanda kwa gharama za mafuta katika soko la dunia kwa hadi 21%, gharama za uagizaji wa mafuta hadi 62% ikilinganishwa na mwezi Agosti, 2023 na maamuzi ya kisiasa katika nchi zinazozalisha mafuta kwa wingi (OPEC+)**. Bei za mafuta katika miji, wilaya na mikoa ni kama zinavyooneshwa katika **Jedwali Na. 1** na bei za mafuta kwa wafanyabiashara wa jumla ni kama zinavyooneshwa katika J**edwali Na. 2.**

Wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa rejareja wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei zinazooneshwa katika Jedwali Na. 1. Aidha, wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei zinazooneshwa katika Jedwali Na. 2. **Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakayekiuka AGIZO hili.**

EWURA inapenda kuwakumbusha wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla na rejareja pamoja na jamii kuzingatia yafuatayo: -

a) bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli kwa eneo husika zinapatikana kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

b) Kwa mujibu wa **Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166,** bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta.

c) Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani isipokuwa **bei hizo zisizidi bei kikomo *(Price cap)* au kuwa chini ya bei iliyoruhusiwa *(Floor Price)* kama zilivyokokotolewa kwa mujibu wa Kanuni za EWURA za Kupanga Bei za Mafuta za Mwaka 2023 zilizotangazwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 421 la tarehe 23 Juni 2023.**

d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana yakionesha bei za mafuta, punguzo, vivutio vya kibiashara vinavyotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

e) Wauzaji wa bidhaa za mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa stakabadhi za mauzo kutoka kwenye Electronic Fiscal Pump Printers (EFPP) na wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora unaotakiwa. Stakabadhi hizo pia zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya bidhaa za mafuta ya petroli.

**JEDWALI 1: BEI KIKOMO ZA REJAREJA KWA SHILINGI/LITA**

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
| **Dar es Salaam** | **3,213** | **3,259** | **2,943** |
| **Arusha** | **3,297** | **3,343** | **3,027** |
| Arumeru (Usa River) | 3,297 | 3,343 | 3,027 |
| Karatu | 3,315 | 3,362 | 3,046 |
| Longido | 3,308 | 3,354 | 3,038 |
| Monduli | 3,302 | 3,349 | 3,033 |
| Monduli-Makuyuni | 3,307 | 3,354 | 3,038 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 3,388 | 3,435 | 3,119 |
| **Coast (Kibaha)** | **3,217** | **3,264** | **2,948** |
| Bagamoyo | 3,224 | 3,270 | 2,954 |
| Bagamoyo (Miono) | 3,254 | 3,301 | 2,985 |
| Bagamoyo (Mbwewe) | 3,235 | 3,282 | 2,966 |
| Chalinze Junction | 3,227 | 3,273 | 2,957 |
| Chalinze Township (Msata) | 3,231 | 3,277 | 2,962 |
| Kibiti | 3,233 | 3,280 | 2,964 |
| Kisarawe | 3,220 | 3,266 | 2,950 |
| Mkuranga | 3,222 | 3,269 | 2,953 |
| Rufiji | 3,240 | 3,287 | 2,971 |
| **Dodoma** | **3,271** | **3,318** | **3,002** |
| Bahi | 3,279 | 3,325 | 3,009 |
| Chamwino | 3,267 | 3,313 | 2,997 |
| Chemba | 3,298 | 3,344 | 3,029 |
| Kondoa | 3,304 | 3,351 | 3,035 |
| Kongwa | 3,269 | 3,315 | 2,999 |
| Mpwapwa | 3,273 | 3,319 | 3,003 |
| Mpwapwa (Chipogoro) | 3,285 | 3,331 | 3,015 |
| Mtera (Makatopora) | 3,290 | 3,337 | 3,021 |
| Mvumi | 3,278 | 3,324 | 3,009 |
| **Geita** | **3,378** | **3,425** | **3,109** |
| Bukombe | 3,367 | 3,414 | 3,098 |
| Chato | 3,399 | 3,446 | 3,130 |
| Mbogwe | 3,416 | 3,463 | 3,147 |
| Nyang'hwale | 3,393 | 3,440 | 3,124 |

## TANGAZO


| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
| **Iringa** | **3,277** | **3,323** | **3,007** |
| Ismani | 3,282 | 3,328 | 3,013 |
| Kilolo | 3,281 | 3,328 | 3,012 |
| Mufindi (Mafinga) | 3,287 | 3,333 | 3,017 |
| Mufindi (Igowole) | 3,295 | 3,342 | 3,026 |
| **Kagera (Bukoba)** | **3,428** | **3,475** | **3,159** |
| Biharamulo | 3,402 | 3,449 | 3,133 |
| Karagwe (Kayanga) | 3,445 | 3,491 | 3,175 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 3,450 | 3,497 | 3,181 |
| Muleba | 3,428 | 3,475 | 3,159 |
| Ngara | 3,416 | 3,462 | 3,147 |
| Misenyi | 3,437 | 3,483 | 3,167 |
| **Katavi (Mpanda)** | **3,370** | **3,417** | **3,101** |
| Mlele (Inyonga) | 3,352 | 3,399 | 3,083 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 3,390 | 3,436 | 3,120 |
| Tanganyika (Ikola) | 3,388 | 3,435 | 3,119 |
| **Kigoma** | **3,375** | **3,422** | **3,106** |
| Uvinza (Lugufu) | 3,365 | 3,412 | 3,096 |
| Muyobozi Village (Uvinza) | 3,374 | 3,420 | 3,104 |
| Ilagala Village (Uvinza) | 3,376 | 3,422 | 3,106 |
| Buhigwe | 3,374 | 3,420 | 3,104 |
| Kakonko | 3,376 | 3,422 | 3,106 |
| Kasulu | 3,384 | 3,431 | 3,115 |
| Kibondo | 3,382 | 3,428 | 3,112 |
| **Kilimanjaro (Moshi)** | **3,286** | **3,333** | **3,017** |
| Hai (Bomang'ombe) | 3,290 | 3,336 | 3,020 |
| Mwanga | 3,279 | 3,326 | 3,010 |
| Rombo (Mkuu) | 3,307 | 3,354 | 3,038 |
| Same | 3,273 | 3,319 | 3,003 |
| Siha (Sanya Juu) | 3,293 | 3,339 | 3,024 |
| **Lindi** | **3,272** | **3,318** | **3,002** |
| Lindi-Mtama | 3,290 | 3,336 | 3,020 |
| Kilwa Masoko | 3,246 | 3,293 | 2,977 |
| Liwale | 3,292 | 3,339 | 3,023 |
| Nachingwea | 3,301 | 3,347 | 3,031 |
| Ruangwa | 3,302 | 3,349 | 3,033 |
| **Manyara (Babati)** | **3,335** | **3,382** | **3,066** |
| Hanang (Katesh) | 3,346 | 3,392 | 3,076 |
| Kiteto (Kibaya) | 3,346 | 3,393 | 3,077 |
| Mbulu | 3,348 | 3,394 | 3,078 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 3,367 | 3,414 | 3,098 |
| **Mara (Musoma)** | **3,378** | **3,425** | **3,109** |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 3,391 | 3,438 | 3,122 |
| Rorya (Ingirijuu) | 3,385 | 3,432 | 3,116 |
| Rorya (Shirati) | 3,393 | 3,440 | 3,124 |
| Bunda | 3,370 | 3,416 | 3,100 |
| Bunda (Kisorya) | 3,382 | 3,429 | 3,113 |
| Butiama | 3,376 | 3,422 | 3,106 |
| Serengeti (Mugumu) | 3,387 | 3,433 | 3,117 |
| Tarime | 3,387 | 3,434 | 3,118 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 3,393 | 3,439 | 3,123 |
| **Mbeya** | **3,320** | **3,366** | **3,050** |
| Chunya | 3,329 | 3,376 | 3,060 |
| Chunya (Makongolosi) | 3,335 | 3,381 | 3,065 |
| Chunya (Lupa Tingatinga) | 3,336 | 3,383 | 3,067 |
| Kyela | 3,336 | 3,382 | 3,066 |
| Mbarali (Rujewa) | 3,304 | 3,350 | 3,034 |
| Rujewa (Madibira) | 3,317 | 3,364 | 3,048 |
| Rujewa (Kapunga) | 3,314 | 3,360 | 3,044 |
| Rungwe (Tukuyu) | 3,329 | 3,375 | 3,059 |
| Busokelo (Iwangwa) | 3,332 | 3,378 | 3,063 |
| **Morogoro** | **3,238** | **3,284** | **2,968** |
| Mikumi | 3,253 | 3,300 | 2,984 |
| Kilombero (Ifakara) | 3,275 | 3,322 | 3,006 |
| Kilombero (Mlimba) | 3,298 | 3,344 | 3,029 |
| Kilombero (Mngeta) | 3,287 | 3,334 | 3,018 |
| Ulanga (Mahenge) | 3,286 | 3,333 | 3,017 |
| Malinyi | 3,296 | 3,343 | 3,027 |
| Kilosa | 3,256 | 3,303 | 2,987 |
| Gairo | 3,256 | 3,303 | 2,987 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 3,248 | 3,295 | 2,979 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 3,238 | 3,284 | 2,968 |
| Turian | 3,263 | 3,309 | 2,993 |

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
| **Mtwara** | **3,285** | **3,332** | **3,016** |
| Nanyumbu (Mangaka) | 3,334 | 3,380 | 3,065 |
| Masasi | 3,311 | 3,357 | 3,041 |
| Newala | 3,317 | 3,364 | 3,048 |
| Tandahimba | 3,310 | 3,357 | 3,041 |
| Nanyamba | 3,310 | 3,357 | 3,041 |
| **Mwanza** | **3,363** | **3,409** | **3,093** |
| Kwimba | 3,381 | 3,427 | 3,111 |
| Magu | 3,371 | 3,417 | 3,101 |
| Misungwi | 3,357 | 3,404 | 3,088 |
| Misungwi (Mbarika) | 3,367 | 3,414 | 3,098 |
| Sengerema | 3,395 | 3,442 | 3,126 |
| Ukerewe | 3,422 | 3,469 | 3,153 |
| **Njombe** | **3,305** | **3,352** | **3,036** |
| Njombe (Kidegembye) | 3,326 | 3,372 | 3,056 |
| Ludewa | 3,343 | 3,390 | 3,074 |
| Makambako | 3,297 | 3,344 | 3,028 |
| Makete | 3,336 | 3,382 | 3,067 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 3,303 | 3,349 | 3,033 |
| **Rukwa (Sumbawanga)** | **3,386** | **3,432** | **3,116** |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 3,386 | 3,432 | 3,116 |
| Kalambo (Matai) | 3,393 | 3,439 | 3,123 |
| Nkasi (Namanyele) | 3,399 | 3,446 | 3,130 |
| Nkasi (Kirando) | 3,409 | 3,455 | 3,139 |
| **Ruvuma (Songea)** | **3,336** | **3,383** | **3,067** |
| Mbinga | 3,349 | 3,395 | 3,079 |
| Namtumbo | 3,341 | 3,388 | 3,072 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 3,359 | 3,405 | 3,090 |
| Tunduru | 3,316 | 3,362 | 3,046 |
| **Shinyanga** | **3,342** | **3,388** | **3,072** |
| Kahama | 3,346 | 3,393 | 3,077 |
| Kishapu | 3,350 | 3,396 | 3,080 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 3,358 | 3,404 | 3,088 |
| Ushetu (Kangeme Village) | 3,364 | 3,410 | 3,094 |
| Salawe | 3,355 | 3,402 | 3,086 |
| **Simiyu (Bariadi)** | **3,360** | **3,406** | **3,090** |
| Busega (Nyashimo) | 3,372 | 3,418 | 3,102 |
| Itilima (Lagangabilili) | 3,360 | 3,406 | 3,090 |
| Maswa | 3,353 | 3,400 | 3,084 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 3,364 | 3,411 | 3,095 |
| **Singida** | **3,303** | **3,350** | **3,034** |
| Iramba | 3,315 | 3,362 | 3,046 |
| Manyoni | 3,288 | 3,335 | 3,019 |
| Itigi (Mitundu) | 3,303 | 3,350 | 3,034 |
| Ikungi | 3,299 | 3,345 | 3,029 |
| Mkalama (Nduguti) | 3,328 | 3,374 | 3,059 |
| **Songwe (Vwawa)** | **3,329** | **3,376** | **3,060** |
| Songwe (Mkwajuni) | 3,336 | 3,382 | 3,067 |
| Ileje | 3,333 | 3,379 | 3,064 |
| Momba (Chitete) | 3,338 | 3,385 | 3,069 |
| Tunduma | 3,333 | 3,380 | 3,064 |
| **Tabora** | **3,321** | **3,367** | **3,051** |
| Igunga | 3,321 | 3,367 | 3,051 |
| Kaliua | 3,334 | 3,380 | 3,065 |
| Ulyankulu | 3,331 | 3,378 | 3,062 |
| Nzega | 3,331 | 3,378 | 3,062 |
| Sikonge | 3,330 | 3,376 | 3,060 |
| Urambo | 3,331 | 3,377 | 3,061 |
| Uyui | 3,327 | 3,374 | 3,058 |
| Mpyagula | 3,352 | 3,399 | 3,083 |
| **Tanga** | **3,259** | **3,305** | **2,989** |
| Handeni | 3,238 | 3,285 | 2,969 |
| Kilindi | 3,273 | 3,319 | 3,003 |
| Korogwe | 3,252 | 3,298 | 2,982 |
| Lushoto | 3,261 | 3,308 | 2,992 |
| Mkinga (Maramba) | 3,273 | 3,320 | 3,004 |
| Muheza | 3,259 | 3,305 | 2,989 |
| Pangani | 3,265 | 3,312 | 2,996 |

**JEDWALI 2: BEI KIKOMO ZA JUMLA (SHILINGI/LITA)**

| Bandari | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 3,080.64 | 3,126.64 | 2,812.34 |
| Tanga | 2,975.68 | 2,952.29 | - |
| Mtwara | 3,011.60 | 3,068.64 | - |

Dkt. James A. Mwainyekule
**MKURUGENZI MKUU- EWURA**





# Madiwani wapiga 'stop' ujenzi wa bustani katikati ya mji

**Na Said Sindo,** GEITA

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Mji wa Geita limeagiza kusimamishwa kwa ujenzi wa bustani ya kupumzikia inayojengwa katikati ya Mji wa Geita, wakisema mwekezaji amekwenda kinyume na makubaliano.

Mwekezaji huyo alitakiwa kujenga majengo madogo ya muda lakini yeye amejenga majengo ya kudumu.

Hoja hiyo iliibuka hivi karibuni katika baraza la madiwani ambako baadhi yao walieleza kuwa makubaliano baina yao na mwekezaji huyo ilikuwa ni kuweka majengo ambayo siyo ya kudumu bali yanayoweza kuondolewa pindi eneo hilo litakapohitajika.

Diwani wa Nyanguku, Elias Ngole alisema: "Haya yalikuwa ni maamuzi ya vikao kuwa kujengwe bustani ili watu wapate vinywaji katika eneo hilo na kujengwa majengo kama choo na jiko dogo, lakini siyo kwa majengo ya kudumu kama alivyofanya huyu mwekezaji na wala siyo maadhimio ya wananchi. Hatupo tayari kuadhibiwa kwa hili"

Diwani wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Zaituni Fundikila alieleza Nipashe kuwa hawakupatiwa barua inayoeleza kuwepo kwa mabadiliko ya maamuzi ya kikao juu ya ujenzi wa majengo ya kudumu na hivyo kabla mwekezaji huyo hajatumia fedha zaidi ni bora asitishe ujenzi kwani kuna muda eneo hilo litahitajika.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Costantine Molandi kupitia kikao hicho aliumuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kusitisha mara moja ujenzi unaoendelea katika eneo hilo.


"Tunahitaji tukienda eneo hilo tukute maandishi ya bomoa au simamisha ujenzi, hatuhitaji kuona ujenzi huo ukiendelea" Alisema.

Nipashe ilimtafuta mwekezaji anayeendelea na ujenzi katika eneo hilo, Hamis Fupi na kusema hajapokea sitisho lolote kutoka Halmashauri wala Ofisi ya Mkurugenzi na kueleza kuwa endapo atapata taarifa ya katazo rasmi kutoka katika ofisi hizo yupo tayari kusitisha mara moja.

"Niliomba kujenga mgahawa na sehemu ya kucheza watoto na niliandika na barua ya kuomba kwenye kutumia tofali kwenye jiko na choo na nikaboresha kwa kutengeneza kitu kizuri wala siyo kwamba kuna vitu vikubwa vilivyojengwa katika eneo hili," alieleza.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Lee Joshua alieleza Nipashe ofisini kwake kuwa agizo la kusitisha ujenzi huo tayari wamelipokea na wamelitekeleza kulingana na matakwa ya baraza hilo.

"Tayari tumeweka sitisho na kwa sasa ujenzi huo hauendelei na kimsingi ipo haja sasa ya madiwani kulitembelea eneo hilo na kuona ni nini kinafanyika katika eneo hilo ili kujua ni kwa jinsi gani maamuzi yao yamefikiwa au yamekiukwa," alieleza Kaimu Mkurugezi huyo.




Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Mwanza ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi (wa tatu kulia), akipokea mfano wa hundi ya sh. bilioni 3.7 kutoka kwa Ofisa Mkuu wa Fedha wa kampuni ya Sotta Mining Ltd, Isaac Lupokela wakati wa hafla ya kuanza kwa malipo ya fidia kwa wananchi walioathiriwa na Mradi wa Mgodi wa Dhahabu wa Nyanzaga, wilayani Sengerema, mkoani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bilioni 3.7/- zafidia wananchi mgodi mpya Nyanzaga

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

KAYA 853 waliokuwa wakimiliki maeneo katika mgodi mpya wa dhahabu Nyanzaga uliopo Kata ya Igalula Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza, wamelipwa Sh. bilioni 3.7 ili kupisha mradi wa uchimbaji wa madini hayo.

Aidha, kati ya wananchi hao kaya 152 wamegoma kutia saini katika makubaliano hayo, huku wakitoa machaguo mawili ya aidha kujengewa nyumba au kulipwa fedha taslimu.

Kaimu Meneja wa Sotta Mining, Isack Lupokela, alieleza kuwa kaya 190 tayari mikataba yao imekamilika na kuchukuliwa na walengwa ambao wamelipwa Sh.bilioni 3.7 na kusema kuwa tayari fedha zao zimewekwa kwenye akaunti zao.

Lupokela alisema walengwa ambao wameshapata ufafanuzi wa stahiki zao na wametia saini mkataba ni 701 kati ya walengwa 853 ambao wanatakiwa kulipwa na kupisha mradi.

Akizungumza na wananchi kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilangi, alisema wananchi ambao wameanza kulipwa fidia wanatakiwa kuanza kujiandaa kupisha mradi huo ili uanze kutekelezwa.

Kadhalika, aliwata wawekezaji hao pindi wanapoanza shughuli za uchimbaji kuzingatia sheria na taratibu za utunzaji wa mazingira ikiwa ni pamoja na kulinda vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na Ziwa Victoria.

"Vilevile hakikisheni mnatoa ajira kwa wananchi wa maeneo haya hususani zile zisizo hitaji ujuzi na kwa zenye ujuzi na utaalamu kama wataalamu wanapatikana hapa Mwanza na maeneo yake hakikisheni wanapata wazawa," alisema

Baadhi ya wananchi ambao wamelipwa fidia hizo walieleza Nipashe kuwa walichagua kujengewa nyumba, lengo likiwa ni kujihakikishia kuwa na makazi ya kudumu jirani na mgodi huo ili kupata fursa zitakazokuwa zikitolewa katika eneo hilo.

Mmoja wa wakazi hao Lucas Masanja alisema: "Ukisaini unaulizwa unahitaji nini? fedha kulingana na tathimini ya mali zako au kujengewa nyumba na kupewa eneo la kufanyia shughuli zako nje ya eneo la mradi huo, hivyo ninaona chaguo la nyumba ni bora zaidi kuliko fedha".

# Ukosefu zahanati wasababisha wajawazito kujifungua njiani

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

WAKAZI wa Mtaa wa Manga Kata ya Mugusu Halmashauri ya Mji wa Geita, wakiwemo wajawazito na watoto wanakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa huduma za afya hali inayosababisha baadhi yao kujifungulia njiani.Hali hiyo inatokana na kutembea umbali wa zaidi ya kilomita tano kufuata huduma katika Mtaa wa Nyakabale.

Walieleza kilio hicho jana kutokana na kutokukamilika kwa zahanati yao ambayo ujenzi wake ulianza mwaka 2020, hali inayowafanya kutumia usafiri wa pikipiki na baiskeli kusafirishia wagonjwa kufuata huduma ya uzazi katika zahanati iliyopo Mtaa wa Nyakabale.

"Wanawake wajawazito tunateseka tunatembea umbali mrefu, wakati mwingine uchungu unatushika nyakati za usiku, kama hauna uwezo kupata usafiri wa pikipiki au baiskeli unalazimika kutembea kwa miguu, unajifungulia njiani unafika zahanati na kondo la nyuma limeshatoka" alisema Shida Joseph.

Naye, Sikitu Madalali alieleza kuwa licha ya huduma hiyo kupatikana mbali bado wajawazito wamekuwa wakiteseka kutokana na miundombinu ya barabara kutokuwa rafiki, hali inayosababisha wanatumia muda mrefu kutafuta huduma za afya.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi mifuko 100 ya saruji iliyotolewa na mwekezaji mzawa wa kampuni ya uchimbaji wa dhahabu Geita Resources, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, John Luhende alisema ametoa mifuko hiyo ili kuunga mkono juhudi za serikali na wananchi katika ujenzi wa zahanati.

Akipokea saruji hiyo Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa huo, Elias Lukanya alisema, kuwa mtaa huo una watoto 113 wenye umri chini ya miaka mitano na wananchi 2,172.

Alisema wajawazito na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano wamekuwa miongoni mwa wanaokabiliwa na adha hiyo kwa muda mrefu, hivyo kuomba wadau kuwasaidia kukamilisha ujenzi huo.



Ukurasa 12

**Kuondoa udhalimu, ubadhirifu kuimarishe udugu na uzalendo**





Ukurasa 13

'Maninja' wa kisiasa wanaoitikisa misingi ya mfumo dume Shinyanga



Ukurasa 14

**Mjeshi aliyechafua fungate la ushindi wa Ali Bongo Gabon**


# siasa

JUMATANO SEPTEMBA 6, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


KINACHOIBUKA DAKIKA 45 ZA MSUYA

# Kasoro za katiba ya sasa zirekebishwe kazi iendelee

• Apinga elimu kutolewa miaka mitatu, umahiri CHADEMA kwa hoja wamkosha

**Na Sabato Kasika**

MOJA ya mambo ambayo yamewaibua watu wa kada mbalimbali na yanayoendelea kujadiliwa, ni Wizara ya Katiba na Sheria kutangaza kuwa itatumia miaka mitatu kutoa elimu ya katiba, kwa Watanzania kwa sababu asilimia 50 hawajui na wengine hawajawahi kuiona.

Kauli hiyo inakutana na upinzani kutoka kila kona unaopinga kuutumia muda huo kuelimisha umma kwa maelezo kuwa ni kupoteza wakati na rasilimali za walipa kodi. Wakati sakata hilo likiendelea, Waziri Mkuu mstaafu, Cleopa Msuya, anaungana na wanaohoji hatua hiyo akisema haoni sababu ya kufanya hivyo, kwa kuwa wananchi wana uelewa kuhusu mchakato huo.

Msuya anasema hayo katika mahojiano ya kipindi cha Dakika 45 cha ITV kinachorushwa kila Jumanne usiku, huku akishauri kufanyiwa marekebisho vifungu vyenye kasoro katika katiba ya sasa.

"Nasikia wamezungumza juzi kuwa ni mabilioni sijui ngapi za kuelimisha watu. Unamuelimisha mtu nini? Kwa mfano ungekuja kule kijijini kwangu unielimisha juu ya katiba unielimishe nini, mfumo gani, kwa maana hakuna katiba ambayo ni 'standard'," anasema Msuya.

Mwanasiasa huyo mkongwe, anaeleza kuwa tatizo sio elimu, na kwamba kama kuna upungufu katiba ya sasa ambao unakwaza watu, urekebishwe kila mara ili kumaliza suala hilo.

"Ninaamini kwamba tusingeweka mipaka kusema tuelimishe watu miaka mitatu, nafikiri tungeweka nini kinapungua katiba ya sasa ambacho kinatakiwa kurekebishwa na tuone jinsi ya kushauriana na kufikia muafaka na tupitishe yaingie katika katiba mpya ambayo itarekebisha hii iliopo ili tuendelee na kazi."



Waziri Mkuu mstaafu, Cleopa Msuya. **PICHA: MTANDAO**

Aidha, anasema hakuna nchi inaweza kuwa na katiba moja kila wakati, lakini pia anasisitiza kwamba jambo la msingi ni kufanya marekebisho katika katiba ya sasa, na kwamba njia hiyo itasaidia kuokoa fedha za walipa kodi, kwa kuwa vikosi kazi vilishaundwa vingi na vimetumia fedha nyingi za walipa kodi.

Mtazamo huo wa Msuya, umefanana na wa Jaji Joseph Warioba ambaye hivi karibuni alikaririwa na vyombo vya habari akisema wakati akiwa Mwenyekiti wa Tume ya Katiba Mpya, walipata elimu hiyo kwa kuwa walisambaziwa nakala za katiba za Tanzania na Zanzibar.

Lakini pia anafafanua kuwa walifanya machapisho kueleza yaliyo katika katiba na kusambaza katika maeneo mbalimbali mijini na vijijini, na kwamba si sahihi kusema wananchi hawana elimu kuhusu mchakato huo.

Jaji Warioba, haoni kama wanaweza kutoa mwanga zaidi kuliko ambao wananchi waliona, na kwamba kikosi kazi cha Profesa Rwekaza Mukandala kilishachukua maoni ya kutosha ambayo wananchi wanaijua.

**MAELEZO YA WIZARA**

Hivi katibuni aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, sasa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, alikaririwa na vyombo vya habari akisema serikali itatoa elimu ya mabadiliko ya katiba kwa miaka mitatu.

Waziri Ndumbaro anazitaja sababu za kutaka kufanya hivyo kuwa ni kutokana na utafiti mbalimbali ambao umefanyika, unaobaini kuwa zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania hawaifahamu katiba na hata wengine hawajawahi kuiona.

Baada ya kauli hiyo, baadhi ya wadau Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC) na Jukwaa la Katiba, waliibuka na kupinga msimamo huo wa serikali.

Kwa mujibu wa wadau hao, ni kwamba msimamo huo unalenga kuchelewesha mchakato wa kupata katiba mpya, huku wakiitaka serikali kuharakisha mchakato na kuachana na elimu.

**MWENENDO KISIASA**

Akijibu swali kuhusu hali ya kisiasa hivi sasa, anasema kufungua milango ya kisiasa vyama kufanya mikutano ya hadhara ni jambo la kawaida na kwa mtazamo wake anaona kama kuna tija kwa taifa wale walioko kwenye vyama wanajitahidi kujenga hoja ili ikiwezekana safari ijayo wachukue dola.

Msuya anasema ni wajibu wa chama tawala nao washuke chini kwa wananchi kujibu hoja zinazoibuliwa na wapinzani, kwa kuwa vinginevyo hoja zinazojengwa wanaweza kujikuta katika wakati mgumu.

"Upende usipende hao watu wa CHADEMA ni wachambuzi wa mambo kwa kina, ni lazima tujifunze kwao, kwanini wanajifunza hivi na kwanini baadhi ya watu wetu hawawezi kujifunza kiasi hicho hadi wategemee upande wa pili," anasema.

Anafafanua kuwa upinzani kutafuta makosa ya viongozi chama tawala na serikali ni lazima ili kujijengea uhalali kwa wananchi, na kwamba watu wanasema CCM imelemaa kwa sababu ya kutegemea zaidi serikali, na kusababisha wasiweze kujifunza mbinu za kujibu hoja.

Katika nyongeza yake, anasema wapinzani lengo lao kutafuta mapungufu na makosa mbalimbali ya watawala, ili kushawishi wananchi kuwanyima kura na kwamba ni muhimu CCM kujua hoja hizo na jinsi ya kuzijibu.

CCM nao wajitahidi ili kuwashawishi wananchi kuwa haya wanayoyasema wanayatekeleza hadi yashuke kule chini.

NA IJE KATIBA MPYA....

# Kuondoa udhalimu, ubadhirifu kuimarishe udugu na uzalendo

**Na Dk. Felician Kilahama**

MCHAKATO wa kutayarisha katiba mpya , umeanza zaidi ya miaka 10 iliyopita, ukiwahusisha Jaji Joseph Warioba na timu yake, wakikusanya maoni kutoka kwa wadau wengi nchi nzima kuanzia Makunduchi Zanzibar hadi Makambako Iringa.

Hata hivyo, kwa sababu ambazo Watanzania wengi hawakuzifahamu, kazi hiyo, imekwama, hivyo jitihada za kuipata zikapungua nguvu, lakini kumekuwepo na vuguvugu na mapendekezo kutoka kwa baadhi ya wadau hususani wanasiasa hasa upinzani kwamba katiba mpya ni muhimu kwa masilahi ya taifa.

Sasa kuna msukumo wa pekee kwamba iwe ni matokeo ya maridhiano na ikamilike kwa matarajio kuwa itatumika wakati wa uchaguzi mkuu 2025. Nia yao ni njema kwa msingi kwamba taifa liwe na uhakika masilahi ya wengi yanalindwa kwa faida ya wote.

Hii ni pamoja na kuona kuwa kuna tume huru ya kuendesha na kuusimamia uchaguzi na kutenda haki. Kadhalika, isiingiliwe na yeyote katika kutimiza majukumu yake kwa kuzingatia misingi ya katiba pamoja na sheria na kanuni zake.

Aidha, wapo baadhi ya Watanzania ambao wangependa kuona wakati wa uchaguzi ujao 'mgombea binafsi' asiyeambatana na chama chochote cha siasa, anachangamkia haki hiyo kikatiba.

Natambua kwamba katiba ndiyo sheria mama au msingi mkuu wa kuendesha na kuisimamia nchi kiutawala na kijamii, kwa hiyo, chochote kingine hakitakiwi, kwa namna yoyote ile, kupingana au kukinzana na katiba .

Isitoshe, nimekuwa nikiona na kushuhudia umuhimu wake kwa taifa letu kuwa viongozi wa juu, ukianzia rais pamoja na wasaidizi wake hasa anaowateua wanakula kiapo kuitetea na kuilinda katiba.

Pamoja na nia njema hiyo, najiuliza hivi wanaitetea na kuilinda au katiba ndiyo inayowatetea na kuwalinda? Hebu tutafakari kwa nia njema ya kuimarisha masilahi na kwa faida ya wengi kutokana na katiba kuwa ndiyo chombo kikuu cha kuliongoza taifa hili.

Tanzania inafahamika duniani kwamba ni nchi huru na salama yenye mipaka inayoeleweka na kuheshimiwa kitaifa na kimataifa. Ndani yake wapo takriban Watanzania milioni 61.7 kwa mujibu wa Sensa, 2022.

Ili nyumba au Tanzania iweze kuwa imara na salama kwa watu waishio humo, ni lazima ijengwe kwenye msingi imara usioweza kusababisha iyumbe hata kama dhoruba kali zikiitikisa iweze kubaki kama ilivyojengwa na kuwahakikishia usalama wanaoishi humo na mali zao.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dk. Eliezer Feleshi. **PICHA: MTANDAO**

> Hili litaleta umakini mkubwa na kuondoa hali ya 'sintofahamu' ambayo baadhi yetu wanaweza kuitumia kama fursa ya kujinufaisha wakati wananchi walio wengi wakiteseka.

Kwa mtazamo huo katiba ya taifa letu ndiyo nguzo kuu na ya msingi ya nyumba yetu, hivyo unatakiwa uwe imara kama ni zege liwe lenye sementi kali, kokoto na mchanga kikamilifu. Isitoshe, usimamizi wake unatakiwa, wakati wote, uwe imara na thabiti na usioyumbishwa na chochote.

Ninachokisema namaanisha katiba tarajiwa ilenge kuimarisha musitakabali mzima wa taifa letu kwa misingi kwamba tuwe na chombo kisichotiliwa mashaka na yeyote na kiwe na thamani ya kutumika muda mrefu hata kama ni zaidi ya miaka 100 ijayo, kwa masilahi ya taifa na raia wake.

Katiba inayotumika leo ilipitishwa 1977 na waliokuwa madarakani kulingana na walivyoelewa wakizingatia mazingira yaliyokuwa wakati huo. Kimsingi, haikuwa mbaya isipokuwa ni huluka kuwa na mitazamo ya mielekeo inayotofautiana ndiyo maana ya kuwapo mahitaji ya nyingine sasa

Tujiulize tunahitaji katiba mpya ili iweje? Kwanza, iwe msingi imara wa kuimarisha umoja wa kitaifa hasa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar . Pili, kiwe chombo cha kuimarisha usalama wa taifa kwa kuzingatia mipaka na vyote vilivyomo ndani yake.

Aidha, ilenge kuondoa udhalimu na ubadhirifu, iimarishe uzalendo ili Watanzania wajitambue na kujivunia taifa lao na siyo kinyume chake.

Vilevile, kwa suala la uzalendo, elimu ya uraia itiliwe mkazo lakini pia kuiandaa katiba mpya ni vema wananchi wakaelimishwa kwanza ili waelewe vya kutosha juu ya umuhimu wake na watarajie nini kupitia katiba ikiwa ndiyo nguzo kuu kulisimamia taifa kwa miaka mingi ijayo.

Ithibati iwe ni kuhakikisha kuwa na katiba iliyo imara kuliongoza taifa kwa muda mrefu na kwa kutenda haki, mathalani, madhaifu kwenye katiba iliyopo, yashughulikiwe ipasavyo. Watanzania tumejifunza mengi wakati wa awamu ya tano Rais John Magufuli,alifariki ghafla muda mfupi baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2020, hali ambayo hatukuitarajia.

Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akaapishwa kwa mujibu wa katiba kuwa Rais. Nilichojifunza ni kwamba, katiba inatoa 'fursa' makamu wa rais, kuwa kiongozi mkuu wa nchi na kujulikana ni serikali ya awamu nyingine bila ya kufanya uchaguzi.

Suala kama hili napendekeza liangaliwe kwa umakini na kuwa bayana kwenye katiba inayotarajiwa kuwa iwapo kifo kitokea kama ilivyokuwa katika awamu ya tano, kikatiba iwe wazi kwamba ndani ya miezi kadhaa baada ya uongozi wa makamu anayeapishwa baada ya kifo kufanyike uchaguzi mkuu ufanyike ili kumpata mtawala aliyetokana na kura nyingi za wananchi na aunde serikali inayotokana na ridhaa ya wannachi.

Hili litaleta umakini mkubwa na kuondoa hali ya 'sintofahamu' ambayo baadhi yetu wanaweza kuitumia kama fursa ya kujinufaisha wakati wananchi walio wengi wakiteseka.

Vilevile, katiba mpya iwe wazi kwa madaraka ya rais maana ya sasa imemrundikia madaraka makubwa kiasi kwamba anafanya kila kitu.

Kadhalika, kwa mashirika na taasisi za umma, katiba iweke wazi kwamba watendaji wakuu (CEO) wasiwe wateule wa rais, bali nafasi hizo zitangazwa na wenye sifa waombe na hatimaye apatikane atakayefaa kusimamia chambo cha umma ipasavyo.

Iwapo shirika litakufa likiwa mikononi mwake awajibishwe ipasavyo kulingana na sheria na kanuni zitakazowekwa, kusiwepo na kupendeleana wala kuingiliwa katika utendaji. Kuwepo chombo cha juu cha kushughulikia taasisi za umma na wajumbe wake wapigiwe kura na bunge kama tunavyofanya kwa wabunge wa Afrika Mashariki.

Vilevile, katiba iwajibike kwa Waziri Mkuu na kufanya kazi kwa muda maalumu ili wapatikane wajumbe wengine na jambo hili lisifanyike kisiasa bali kwa kuzingatia misingi ya utendaji bora na wenye kuleta tija kubwa kwa taifa.

Madaraka ya wananchi ni pamoja na kuiweka serikali kutawala. yawe bayana katika katiba kwa faida yetu wote. Utashi wa viongozi wakuu serikalini na wanasiasa waandamizi kufanya wanavyoona inafaa, hata kama wanachotaka kukifanya hakina masilahi kwa wananchi viepukwe.

Katiba iwe 'muarobaini' kwa masuala kama hayo. Taifa lisitumbukizwe kwenye 'mitego' yenye taswira ya 'kuwaletea maendeleo wananchi', wakati wakijua ni kwa masilahi ya watu wachache.

Kanuni muhimu iliyokuwa ikiwazuia watunga sera na wasimamizi wa shughuli za serikali kutojihusisha na biashara, ilifutwa. Hivyo, wahusika sasa wako huru kufanya wanavyotaka. Kwa halihiyo, Watanzania tunakabiliwa na changamoto kubwa kuhusu "migongano ya kimasilahi" (conflict of interests).

Haiwezekani kuhudumia 'mabwana wawili' utampendelea mmoja na kumdhoofisha mwingine , kadhalika ni vigumu kusimamia sera, sheria na kanuni kikamilifu kama una upande unaoutetea maana "hazina ya mtu ilipo ndipo moyo huegamia".

**ITAENDELEA WIKI IJAYO**

MARIAM & ZAMDA

# 'Maninja' wa kisiasa wanaoitikisa misingi ya mfumo dume Shinyanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MFUMO dume au taratibu, mazoea na desturi zinazowakandamiza wanawake wakati huo zikiwainua na kuwaenzi mara zote wanaume, umeendelea kuwa jambo linaloongeza ukosefu wa usawa kwenye sekta na hali zote ndani ya jamii.

Ni jambo linalopigiwa kelele na wadau mbalimbali wakiwamo wanaharakati, wakipigania kutoa fursa na nafasi kwa wanawake kushika majukumu ya kiuongozi na kufikia usawa wa kijinsia.

Shinyanga ni miongoni mwa mikoa ambayo imekuwa ikiutukuza mfumo dume, hata kushindwa kuwapigia kura za ndiyo wanawake kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, mkuu na hata ule unaofanyika kwa minajili ya kupata viongozi kwenye maeneo mbalimbali.

Mwaka 2019, Tanzania ilifanya uchaguzi wa serikali za mitaa na katika manispaa ya Shinyanga kinamama wengi ilikuwa vigumu kunusa ushindi, kadhalika na uchaguzi mkuu 2025 kwa nafasi za udiwani na ubunge ilikuwa ngumu ikilinganishwa na idadi ya wanaume.

Msimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019 katika Manispaa ya Shinyanga Charles Kafutila, anasema vipo vijiji 17, lakini hakuna mwanamke aliyeshinda nafasi hiyo.

Anasema kwa nafasi ya wenyeviti wa vitongoji 84, wanawake waliambulia viti nane pekee na wanaume walikomba vyote 76, kadhalika uchaguzi mkuu 2020 udiwani, ndani ya kata 17, lakini wanawake walioshinda nafasi hiyo wawili ambao ni kata ya Kitangiri Mariam Nyangaka na Zamda Shaaban wa Ndala.

Tatizo hili la wanawake kushindwa katika chaguzi hizo na kukosa nafasi za uongozi, linatokana na jamii kutawaliwa na mfumo dume na kutowaamini wanawake kama wanaweza kuwa viongozi na kuwaletea maendeleo, anasema Kafutila na kwamba madiwani hao kutoka CCM, wanaongoza kata ambazo awali zilikuwa chini ya CHADEMA,

Diwani wa Ndala Zamda, akizungumza na Nipashe kuhusu mafanikio yaliyopatikana uongozi wake, anakiri kuwa bado baadhi ya wanaume wanambeza kuwa hafai kwa vile ni makuwadi wa mfumo dume, licha ya kushirikiana na wananchi kuwaaletea maendeleo.

Anatamba kutatua changamoto ya ubovu wa miundombinu ya barabara kwamba ameshirikiana na wananchi na halimashauri kufanikihs kuchonga kilomita 13, kufungua barabara mpya zenye urefu wa kilomita sita, ujenzi wa makalavati zaidi ya 15 na amejenga daraja la watembea lenye thamani ya Shilingi milioni 100 ili wasipite daraja la magari na kuepusha ajali.

Anasema pia kujenga shule mpya ya Msingi Msufini 'B', ujenzi wa madarasa saba ya Sekondari Ndala, matundu 10 vyooni na chumba cha kujistiri wakati wa hedhi na kwamba halmashauri pia amelipa fidia eneo ambalo itajengwa zahanati ya Ndala fedha zilizoshindikana kulipwa zaidi ya miaka 10 na kuahidi kuwa ujenzi utaanza mwaka huu.





Mariamu Nyangaka wa Kitangiri na Zamda Shaaban (mwenye mavazi ya bluu) wa kata ya Ndala. **PICHA: MARCO MADUHU**

> Sifa ya mtu ili uwe kiongozi bora, lazima ujiamini, kusoma katiba ya chama chako, ya nchi pamoja na kufanya utafiti ili ujue ni matatizo gani makubwa ambaye ni kero kwa wapigakura na kuzitatua ukifanya hivyo huwezi kushindwa kuongoza.

Kwa upande wa ukarabati wa soko la Ndala ambalo limekufa miaka mingi, anasema tayari halmashauri imetenga Shilingi milioni 40 kwa ajili ya kufanyiwa maboresho na kuanza kutumika, huku akishirikiana na viongozi kutatua pia tatizo la kukosa umeme kwa wapigakura walio pembezoni mwa kata yake kwa kuanza kuwekewa nguzo za umeme.

"Kata hii ya Ndala ilikuwa na changamoto nyingi kimaendeleo kwa miaka mingi, na nilivyoshinda udiwani watu wengi walinibeza kwamba sitaweza kubadilisha hali hiyo sababu ni mwanamke, lakini kwa juhudi hizi nimewafunga midomo hawana cha kusema tena,"anasema Zamda.

Anataja siri ya mafanikio yake ya kushinda udiwani kwa mara ya kwanza na kisha kuchaguliwa kuwa Naibu Meya wa Manispaa ya Shinyanga, kuwa ni kuchapakazi, kusikiliza kila mtu bila kujikweza, ndiyo maana ameaminiwa na wananchi na madiwani wenzake waliompa jukumu la Naibu Meya.

Diwani wa Kitangiri Mariamu Nyangaka ambaye naye aliyeshinda nafasi ya hiyo uchaguzi wa 2020, akiing'oa CHADEMA, anasema ndani ya miaka yake mitatu amefanya maendeleo makubwa na wanaume wameanza kumwamini mwanamke kuwa anaweza kuwaongoza.

Anasema kata hiyo ya Kitangiri tangu nchi ipate uhuru mwaka 1961 ilikuwa ikiongozwa na madiwani wanaume, na yeye ndiye wa kwanza mwanamke kupitia CCM, na amekuwa kiongozi anayeisimama na matatizo ya wananchi.

Anataja baadhi ya juhudi za maendeleo anazofanya kuwa ni kushirikiana na wananchi kutengeneza barabara ya changarawe yenye kilomita 34 na madaraja matatu ambayo yalikuwa sehemu korofi kwa miaka mingi pamoja na kuweka mitaro na makalavati.

Kadhalika, ameshirikiana na viongozi na yamejenga zahanati, shule mpya ya Kitangiri 'B', upatikanaji wa huduma za maji na umeme ni mambo aliyoyavalia njuga.

Anasema katika zahanati matarajio yake kwa miaka ijayo ni kuipanua kuwa kituo cha afya, kutokana na eneo hilo kuwa na wananchi wengi wanaotegemea huduma hapo pamoja na kujenga soko kubwa.

"Changamoto za kubezwa kama kiongozi mwanamke hazikosekani sababu ya jamii kutawaliwa na mfumo dume, lakini tunasonga mbele anasema,"anasema Mariam.

"Uchaguzi mkuu ujao 2025 nitagombea tena udiwani sababu bado malengo yangu hayajatimia ya kuibadilisha Kitangiri, nawaomba tu wapigakura wangu waniamini na kunichagua tena niwatumie na kuwaletea maendeleo,"anaongeza.

Habiba Ramadhani ni miongoni mwa wenyeviti wa mitaa kati ya wanawake sita ambao walishinda kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2019 Kitangiri, anasema wanawake wakipewa nafasi ni viongozi ni wazuri na wachapakazi.

Anasema alianza kugombea nafasi ya hiyo tangu mwaka 2014 na 2019 akashinda tena kutokana na wananchi kumwamini utendaji wake kazi, na amekuwa wakishindana na wanaume na kuwashinda.

"Sisi wanawake kwanza hua tunahuruma sana tofauti na wanaume ndivyo tulivyoumbwa, sasa ukiona wananchi wako wanateseka na kitu flani unaumia zaidi itabidi upambane hadi kitatuliwe, naiomba tu jamii iendelee kutuamini wanawake ni viongozi bora tutawaletea maendeleo,"anaahidiHabiba.

Siri Yasini ni Mwenyekiti ACT-Wazalendo mkoani Shinyanga, anasema katika chama hicho wanathamini sana uwasawa wa jinsia na wanawake ambao wanasifa za kuwa viongozi wamekuwa wakipewa nafasi za kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika chaguzi ndani ya chama na uchaguzi wa serikali za mitaa hadi mkuu.

"Sifa ya mtu ili uwe kiongozi bora, lazima ujiamini, kusoma katiba ya chama chako, ya nchi pamoja na kufanya utafiti ili ujue ni matatizo gani makubwa ambaye ni kero kwa wapigakura na kuzitatua ukifanya hivyo huwezi kushindwa kuongoza,"anasema Siri.

Mzee wa Kimila Sonda Kabeshi, anasema tatizo la mfumo dume ni urithi wa mababu kutoka enzi na enzi, na ni moja ya mila na desturi ambayo iliwekwa kwamba wanaume ndiyo viongozi wa kila kitu na mwanamke atabaki kuwa msaidizi na siyo kiuongoza mwanaume.

Anasema mila hizo zimekuwa zikidumaza wanawake na kuwa dhaifu katika masuala ya uongozi, na hata kuzungumza kwenye mikutano walipo wanaume ni marufuku hata kama wana jambo lao.

Anaeleza kuwa zamani mwanamke akiwa kiongozi anaweza kutengwa hata ukweni au mji kuvunjika kwamba atamdharau mumewe, huku akionekana ndani ya jamii kama jeuri

"Sasa hivi jamii imeanza kubadilika na kuwakubali wanawake kuwa viongozi sababu ya kutolewa elimu ya usawa wa kijinsia, na mabadiliko haya hayahitaji haraka ni taratibu, tamaduni hizi kubadilika haihitaji nguvu na tunaona wanawake waliopata nafasi wanachapa kazi sana,"anasema Kabeshi.

JUKWAA LA VIONGOZI

JENERALI BRICE NGUEMA

# Mjeshi aliyechafua fungate la ushindi wa Ali Bongo Gabon

• Alisubiri pale tume ya uchaguzi ilipompa ushindi



Jenerali Brice Oligui Nguema

**Na Christina Mwakangale**

AFRIKA inatikisa dunia ikiwa ndilo bara lenye matukio mengi ya mapinduzi ya kijeshi ya kuzing'oa madarakani serikali zinazodaiwa kuwa ni za kimila zinazojipachika madaraka kupitia wizi kwenye sanduku la kura.

Mwaka huu imeshuhudia mikasa kadhaa ya mapinduzi ya kijeshi na hivi karibuni ni kutumbuliwa kwa Ali Bongo Rais wa Gabon, anayerithi utawala kutoka kwa baba yake Omary Bongo, aliyetawala kwa miongo minne.

Dunia imeshuhudia mapinduzi 18 kuanzia mwaka 2017 na kati ya hayo 17 yamefanyika Afrika na moja nchini Myanmara (Burma) barani Asia.

Gabon, nchi iliyopo Afrika ya Kati, wiki iliyopita imetia fora siku chache baada ya taifa hilo, kufanya uchaguzi uliomrejesha madarakani Rais Ali Bongo kwa muhula wa tatu, jeshi likamtumbua.

Mapinduzi hayo yanajiri siku kadhaa baada ya walinzi wa Rais wa Niger Mohamed Bazoum kumpindua kiongozi huyo aliyechaguliwa kidemokrasia.

Ali Bongo, anaondolewa madarakani na Jenerali Brice Oligui Nguema, ambaye alibebwa barabarani na wanajeshi wenzake wakiimba Oligui, rais, Oligui, rais.

Miezi minane iliyopita, Jenerali Nguema alitoa kiapo cha utii na uaminifu wake mbele ya hadhara, kwa Bongo lakini Alhamisi iliyopita Agosti 30, hakufanya ajizi huu alimtoa rais aliyedumu kwa miaka 14 madarakani.

Saa chache baada ya Ali Bongo kutangazwa kuwa mshindi wa uchaguzi wa urais, jeshi lilitangaza kufuta matokeo na kuchukua hatamu.

> Mwaka 2021 mataifa ya Mali, Chad, Guinea, Sudan na Niger, yalipitia msukomsuko wa kijeshi huku 2022 mapinduzi na mawili yakifanyika Burkina Faso.



Ali Bongo, aliyekuwa rais wa Gabon. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Rais akiwa chini ya kizuizi cha nyumbani, Jenerali Nguema, aliteuliwa kuwa kiongozi wa mpito wa Gabon na amekwishaapishwa na Jaji Mkuu Luke Malaba katika sherehe zilizohudhuriwa na viongozi kadhaa wa Afrika wakiwamo, Marais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa na Filipe Nyusi wa Msumbiji.

Jenerali huyo analiambia gazeti la Le Monde la Ufaransa kwamba watu wa Gabon wametosheka na utawala wa Ali Bongo, na kwamba hakupaswa kuwania muhula wa tatu.

"Kila mtu analalamikia hili lakini hakuna anayechukua jukumu," anasema, "Kwa hiyo jeshi liliamua kufungua ukurasa."

Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU) na Ufaransa, zimelaani mapinduzi hayo, ambayo ni ya nane kufanyika Afrika Magharibi na Kati tangu mwaka 2020.

Pamoja na Jenerali Nguema, kuonekana kuungwa mkono na sehemu kubwa ya umma, amefanikiwa kuunganisha jeshi, ambalo limegawanyika kwa misingi ya kikabila. Akiwa mtu ambaye ametuhumiwa kwa rushwa na kufanya kazi kwa muda mrefu katika utawala wa Rais Ali Bongo, huenda asiwe tumaini jipya kwa watu wa Gabon.

Hata hivyo, ataandikwa katika vitabu vya historia ya nchi kama mtu aliyefungua ukurasa, kwa sababu utawala huo wa Rais Ali Bongo, ungefaulu kwa muhula huu wa tatu, familia ingekuwa imetawala kwa zaidi ya miaka 55, baada ya kutwaa madaraka mwaka 2009 kutoka kwa baba yake Omar Bongo, aliyeishi ikulu kuanzia 1967 hadi kifo chache.

Tume ya Uchaguzi Gabon, ilimtangaza Ali Bongo kuwa mshindi wa uchaguzi kwa kupata asilimia 64.27 ya kura.

Mpinzani mkuu wa Ali Bongo ambaye ni Albert Ondo Ossa, alipata asilimia 30.77 ya kura, akisema tume hiyo iliyosimamia uchaguzi mkuu Agosti 26. Gabon yenye watu karibu milioni 2.3 wengi wao wanaishi kwenye lindi la umaskini.

### CHANZO KUPINDUANA

Mapinduzi ya kijeshi yaliyotikisa barani hapa hata vurugu zinazoamsha maandamano, moja ya sababu zinatajwa kuwa ni kutokana na viongozi kushindwa kuleta maendeleo na kumaliza umaskini. Wengi kuendeleza ubadhirifu, ufisadi na matumizi mbaya ya rasilimali za taifa yanayonufaisha wana familia pekee na marafiki zao hasa mabeberu.

Mapinduzi ya mwanzo Afrika yalianzia Ghana, wakati huo Rais Kwame Nkrumah akipinduliwa mwaka 1966, kuangusha serikali kuliendelea miaka 1980, na hata ilipofika miaka ya 2020 bado.

Mwaka 2021 mataifa ya Mali, Chad, Guinea, Sudan na Niger, yalipitia msukomsuko wa kijeshi huku 2022 mapinduzi na mawili yakifanyika Burkina Faso.

### VINARA MAPINDUZI

Sudan ndilo taifa kinara wa mapinduzi barani, ikipitia mapinduzi 17 mojawapo ni kung'olewa madarakani Rais Omar Al Bashir, mwaka 2019.

Burkina Faso, ilimshuhudia Luteni Kanali, Paul-Henri Damiba, ambaye Januari mwaka 2022, aliingia madarakani kwa mtutu wa bunduki, lakini akang'olewa kwa mtutu miezi michache ya kuiongoza nchi hiyo.

Alianza kwa kumuondoa Rais Roch Kabore, kabla ya mapinduzi milio ya risasi ilirindima, ikisikika usiku kucha karibu na ikulu ya rais na kwenye kambi katika mji mkuu wa nchi hiyo, Ouagadougou.

Oktoba, mwaka jana, ikawa zamu yake Luteni Damiba, baada ya Kapteni Ibrahim Traore wa Jeshi Burkina Faso, kutangaza katika televisheni ya taifa, kuwa amempindua kiongozi huyo wa kijeshi. Kapteni Traore, alieleza sababu ya kuidhinisha mapinduzi hayo ni kutokana na kushindwa kwa Luteni Damiba kukabiliana na waasi.

Halikadhalika Guinea-Bissau, Rais Umaro Sissoco Embalo, alitangaza kunusurika katika jaribio la kupinduliwa, ambalo lilisababisha vifo vya watu na kusema sasa hali ilidhibitiwa

Akiwaambia wanahabari kwamba alikabiliwa na milio ya risasi na silaha nzito kwa takribani saa tano, akiwa na mshauri wa kijeshi, waziri na walinzi wawili katika mji mkuu, Bissau.

Guinea-Bissau ilikabiliwa na mapinduzi ikidaiwa sababu ni vitendo vya rushwa na magendo ya dawa ya kulevya.

Kwa ukanda wa Afrika Mashariki, Burundi imeongoza kwa historia ya mapinduzi huku ikipitia matukio 11. **MITANDAO**



## Serikali kulitangaza jiwe linalocheza, mapango ya Handebezya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema inaendelea kutekeleza mikakati inayolenga kukuza na kutangaza vivutio vya utalii katika Kisiwa cha Ukerewe mkoani Mwanza ikiwamo mapango ya Handebezya na jiwe linalocheza.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dastan Kitandula alitoa ufafanuzi huo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Ukerewe (CCM), Joseph Mkundi.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji nini mkakati wa serikali wa kuvifanya vivutio vya mapango ya Handebezya na Jiwe linalocheza kuwa na tija kwa taifa.

Akijibu swali hilo, Kitandula alisema mikakati hiyo ni pamoja na kutangaza vivutio hivyo kwa kutumia vyombo mbalimbali vya habari.

"Mathalan, Wizara kupitia Bodi ya Taifa ya Utalii (TTB) iliratibu ziara ya kituo cha Televisheni cha ITV kwenda kutembelea baadhi ya vivutio vya utalii vilivyopo Ukerewe vikiwemo mapango ya Handebezya na jiwe linalocheza kwa ajili ya kuandaa documentary (makala maalum) ambayo itakapokamilika itaonyeshwa katika Kituo cha ITV katika kipindi kitwacho 'Chetu ni chetu,'" alisema.

Aidha, alisema mafunzo yanaendelea kutolewa kuhusu uanzishwaji wa utalii wa utamaduni ambapo hadi sasa kuna vikundi vya utalii wa utamaduni vikiwamo Ukerewe na Nansio.

Alisema Wizara hiyo imeendelea kushiriki katika maonesho na matamasha mbalimbali yakiwemo Maonesho ya biashara ya Afrika Mashariki na Tamasha la Bulabo yanayofanyika katika Kanda ya Ziwa kwa lengo la kutangaza vivutio vya utalii na fursa za uwekezaji zilizopo katika ukanda huo.

Kadhalika alisema; "Wizara itaendelea kuhamasisha uwekezaji wa miundombinu inayoelekea katika maeneo yenye vivutio vya utalii, ujenzi wa huduma za malazi zenye hadhi pamoja na kuboresha huduma za kijamii, ikiwemo maji, umeme, huduma za kibenki na mawasiliano".

# Dk. Shoo awapa somo madaktari kuhusu maadili kazini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ASKOFU Mkuu Mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk.Fredrick Shoo, amewaasa madaktari wakristo nchini kujiepusha na mienendo inayochafua maadili yao na kanisa ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa 86 wa mwaka wa Chama Cha Madaktari Wakristo Tanzania (TCMA).

Kiongozi huyo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), alisema ni muhimu sana kujiepushe na vitendo vya rushwa na lugha mbaya katika kuwahudumia wananchi.

"Ninawaasa kuzingatia maadili ya kikristo, muendelee kutoa huduma kwa weledi kulingana na taaluma yenu na pia mzingatie masuala ya ufanisi na ubora wa huduma."

"Pia litakuwa jambo jema iwapo mtaepuka mienendo inayochafua maadili ya udaktari na kuchafua kanisa na taaluma ya afya kwa ujumla,"alisema.

Alisema kazi ya kuwahudumia wagonjwa ni kazi ya wito, hivyo wanapaswa kufanya kazi kwa moyo wa kuthamini maisha ya binadamu, kujituma bila kushawishika au kuwa na tamaa ya kujinufaisha. "Mmepewa dhamana na mnao wajibu mkubwa wa kutunza heshima ya taaluma yenu,"alisema.

Kadhalika, alisema viongozi wa makanisa wataendelea kushirikiana na serikali kusimamia, kuimarisha na kuboresha mahusiano.

Alisema hatua hiyo ni pamoja na kuzipatia suluhisho kero zilizopo ikiwamo ucheleweshaji wa fedha za busket fund na uhamishaji wa watumishi kutoka vituo vya kanisa kwenda vituo vya serikali bila maelewano, kufuata taratibu na kusababisha uhaba wa watumishi unaosababisha kuzorota kwa huduma katika vituo husika.

"Kanisa kupitia Tume ya Kikristo ya Huduma za Jamii (CSSC) limeendelea kushirikiana na serikali kupitia Wizara ya Afya na TAMISEMI katika zoezi la kuandaa sera na miongozo inayotumika katika kuboresha kuimarisha mahusiano na ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi (PPP)," alisema.

Aliomba kupitia mkutano huo wajadili kikamilifu na kuweka mikakati ya kuweza kuwa makini na ufuatiliaji wa mambo ya msingi na uwajibikaji katika hospitali zao.

"Ninatarajia maazimio ya mkutano huu yatatumika katika kuboresha yale mapungufu yaliyopo kwa pamoja na kuhakikisha huduma za afya zinazotolewa na kanisa zinaboreshwa zaidi na kuwa za mfano na endelevu katika jamii. Aidha ninatoa rai kwa TCMA kwa kushirikiana na CSSC kutengeneza mpango wa utekelezaji wa maazimio ya mkutano huu,"alisema.

Naye, Rais wa TCMA, Dk. Paul Kisanga, aliomba uongozi wa makanisa kupitia makatibu wakuu na makatibu wa afya wa majimbo na dayosisi kwa kushirikiana na CSSC kufuatilia kwa karibu suala la fedha za basket fund kwa wakurugenzi wa halmashauri husika kulingana na mikataba yao.

Pia, alishauri kuwapo na mkakati dhabiti wa kuzifanyia ukarabati hospitali na vituo vya kutolea huduma vya kanisa kwa kuboresha vifaa tiba ili kuongeza ufanisi na kuhimili ushindani wa soko.

Kadhalika, Mkurugenzi wa Mtendaji wa CSSC, Peter Maduki, alisema tume hiyo imetekeleza maelekezo ya bodi ya kuanzisha mfuko wa uwekezaji wa afya ili kuondokana na kero za kukosa fedha za kulipa mishahara, kununua dawa na vifaa tiba.



Spika wa Bunge mstaafu na Mbunge wa Kongwa, Job Ndugai (wa pili kulia), Mbunge wa Bahi, Kenneth Nollo (wa pili kushoto) na Mbunge wa Mpwapwa, George Malima (kushoto), wakimsikiliza Meneja Masoko na Mawasiliano wa Lake Energies Group, Matina Nkurlu (kulia), wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kampuni hiyo ya "Kumtua Mama Kuni Kichwani" kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), jijini Dodoma juzi, yenye lengo la kusambaza mitungi ya gesi 13,500 kwa mikoa ya Dodoma, Mwanza, Geita, Morogoro na Arusha, ili kutunza mazingira kwa kupunguza kama si kutokomeza kabisa utumiaji wa nishati ya kuni na mkaa nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi mikoa mitano wapewa mitungi ya gesi, majiko

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WANANCHI wa mikoa ya Dodoma, Morogoro, Mwanza, Arusha na Geita wamepewa msaada wa mitugi ya gesi na majiko 13,500 ili iwasaidie kuondokana na matumizi ya nishati ya kuni na mkaa.

Msaada huo umetolewa na Kampuni ya Lake Energies Group, pamoja na uzinduzi wa kampeni maalum iitwayo 'Mtue mama kuni kichwani'

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo jijini Dodoma jana, Meneja Masoko na Mawasiliano wa kampuni hiyo, Matina Nkurlu, alisema kuwa uamuzi huo umelenga kuunga mkono jitihada za serikali ya utunzaji mazingira kwa kupunguza kama si kutokomeza kabisa utumiaji wa nishati ya kuni na mkaa.

"Lake Energies tumeona ni vyema kuunga mkono jitihada za Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), katika kampeni ya utunzaji mazingira na tayari tumeshasambaza mitungi katika mikoa ya Arusha, Morogoro, Mwanza na Geita.

"Pia, kampeni hii inalenga kumwondolea mwanamke wa kitanzania adha ya kutumia muda mwingi kwenda kutafuta kuni au mkaa wa kupikia na hivyo kuepukana na hatari za huko maporini na badala yake kupata muda mwingi wa kutunza familia na ndoa zao," alisema Nkurlu.

Akizungumza kwa niaba ya wabunge wenzake ambao majimbo yao yamehusishwa katika kampeni hiyo, Mwenyekiti wa wabunge Mkoa wa Dodoma, Job Ndugai, aliishukuru Lake Energies kwa mpango huo, akizitaka kampuni zingine kuiga mfano huo wa kumuunga mkono Rais Samia.

"Kwa niaba ya wabunge wenzangu wa Mkoa wa Dodoma, tunawashukuru sana Lake Energies kwa uamuzi wenu huu wa kuamua kugawa mitungi ya gesi kwa kinamama wa mkoa wetu kwa kushirikiana na serikali yetu.

"Kama ilivyo kwa mikoa mingine, kinamama wa Dodoma wamekuwa wakitumia muda mwingi kwenda kutafuta kuni za kupikia hali inayowachosha, lakini pia ikichangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira. Tunawashukuru sana," alisema Ndugai ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Kongwa.

Mbunge wa Geita, Joseph Musukuma, alisema msaada huo umekuja wakati mwafaka ambao serikali imeonekana kuwajali wanawake kwa kuwapunguzia kama siyo kutokomeza baadhi ya kero zinazowakabili, ikiwamo ya kutumia muda mwingi kutafuta kuni na mkaa wa kupikia.

"Kwa niaba ya wanawake wa Geita, tunawashukuru sana kwa kutufikiria katika kampeni yenu hii, Mungu awabariki sana," alisema Musukuma.

Naye mwakilishi wa REA, Injinia Michael Kyessi, aliwataka Watanzania kubadilika kwa kugeukia matumizi ya gesi kwa kupikia na shughuli nyinginezo zinazohitaji nishati ya moto badala ya kuni na mkaa.





# Spika Tulia atoa msaada kwa mwenye ulemavu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson ametoa msaada wa kiti mwendo kwa kijana, Samwel Mwanizuwa mkazi wa Mtaa wa Maendeleo B katika Kata ya Kalobe jijini Mbeya, ambaye ni mlemavu wa viungo kwa ajili ya kumsaidia kwenye shughuli zake.

Msaada huo uliwasilishwa juzi kwa kijana huyo na Ofisa Habari wa Taasisi ya Tulia Trust inayomilikiwa na Dk Tulia, Joshua Mwakanolo kufuatia ombi la familia hiyo lililowasilishwa kwa Spika alipokuwa jimboni humo.

Mwakanolo alisema Dk. Tulia alipokea ombi la familia ya kijana huyo na akaahidi kukinunua kiti hicho na kukikabidhi na hivyo baada ya kukinunua akaagiza wapeleke ili kimsaidie kijana huyo pamoja na familia yake.

"Hii ni ahadi ambayo Spika mwenyewe aliahidi baada ya kupata taarifa ya kijana huyu, tunaamini kwamba kiti hiki kitamsaidia kijana huyu pamoja na familia yake hasa anapofanya shughuli zake," alisema Mwakanolo.

Aliwataka wananchi wa maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya kutowaficha watoto wenye ulemavu na badala yake wawasaidie kupata mahitaji yao muhimu kama ilivyo kwa watoto wengine wasiokuwa na ulemavu.

Pia, aliwataka kutoa taarifa za watu wenye ulemavu ambao wanahitaji msaada kama huo kutoa taarifa kupitia kwa viongozi wa maeneo yao ili taasisi hiyo iwafikie kirahisi.

Akizungumza baada ya kupokea kiti hicho, Samwel alisema kiti hicho kitamsaidia kutembea umbali mrefu zaidi kuliko alivyokuwa akitembea awali ambapo alikuwa anatembelea magoti.

Alisema atakitumia kiti hicho kwenda kwenye maeneo mbalimbali kufanya shughuli zake za kujipatia kipato na kuisaidia familia yake kupata riziki.

Alimshukuru Dk. Tulia kwa kumpatia msaada huo, huku akimuomba aendelee kuwasaidia watu wengine wenye ulemavu kama yeye.

"Namshukuru sana Dk. Tulia kwa msaada huu wa kiti mwendo, mungu ambariki na naomba aendelee na moyo wake huo wa kuwasaidia watu wenye uhitaji kama mimi," alisema Samwel.

Mama mzazi wa Samwel, Elizabeth Mwalyambi alimshukuru Dk. Tulia kwa kuisaidia familia yake kupata kiti hicho kwa ajili ya kijana wake akidai kuwa kabla ya kupata kiti hicho alikuwa anapata shida kutambaa.

Alisema wakati mwingine ilikuwa ni hatari kwa kijana huyo kupata magonjwa kutokana na kutambaa akidai kuwa alikuwa anaweza kushika vitu vichafu.

Baadhi ya wananchi wa eneo hilo waliwataka watu wengine wenye uwezo kuwasaidia watu wenye uhitaji kwa vitu mbalimbali kama ambavyo Dk. Tulia amekuwa akifanya.

Mmoja wa wananchi hao, Gipson Sheyo alisema kuwasaidia watu wenye uhitaji ni sawa na kutoa sadaka kanisani na hivyo akawataka watu wengine kujitolea.

Alisema watu wenye ulemavu wana mahitaji mengi ikiwemo chakula, malazi na hata mavazi na kwamba watu wengi wamekuwa wakiwasaidia watoto yatima na wazee ambao wanaishi kwenye vituo na kuwasahau walioko mitaani.



Ofisa Habari wa Taasisi ya Tulia Trust, Joshua Mwakanolo (kushoto), akizungumza na kijana mwenye ulemavu wa viungo, Samwel Mwanizuwa mkazi wa Mtaa wa Maendeleo B, Kata ya Kalobe, baada ya kumkabidhi msaada wa kiti mwendo kwa niaba ya Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Bosi Uhamiaji aanza kazi ukaguzi SIA, Kituo cha Forodha

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

OFISA Uhamiaji Mteule wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Uhamiaji, Filbert Ndege ameanza ziara katika maeneo mbalimbali mkoani hapa kwa lengo la kujitambulisha na kuangalia utendaji kazi wa askari.

Katika ziara yake ya kwanza Kamishna Msaidizi wa Uhamiaji, Ndege alitembelea Kituo cha Pamoja cha Forodha Kasumulu (OSBP) kilichopo wilayani Kyela pamoja na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA).

Akizungumza na askari na maofisa wa uhamiaji wa vituo hivyo, aliwataka kutekeleza maagizo mbalimbali yaliyotolewa na Kamishna Generali wa Uhamiaji, Anna Makakala ikiwemo kutoa huduma bora kwa wananchi pamoja na kukusanya maduhuli ya serikali kwa weledi.

Aidha, aliwataka askari na maofisa wa maeneo hayo kuwa na uhusiano mzuri na vyombo vingine vya usalama wakati wa kutekeleza majukumu yao pamoja na kuepuka vitendo vya rushwa.

"Huu mkoa wetu ni miongoni mwa mikoa ambayo iko mipakani kwahiyo lazima tufanye kazi kwa weledi mkubwa sana kuhakikisha wananchi wanapata huduma wanayostahili kutoka kwetu," alisema Ndege.

Aliwataka maofisa hao kuhakikisha wanadhibiti pia wahamiaji haramu ambao wamekuwa wakitoka katika mataifa mbalimbali na kuingia nchini bila vibali.

Katika hatua nyingine alikagua uchakavu wa majengo ya ofisi na nyumba za watumishi katika Wilaya ya Kyela na kuahidi kuendelea kushughulikia.

# Aliyewahi kuwa mbunge Mbeya aibukia uchaguzi Mbarali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADA ya kukaa kimya kwa muda mrefu, aliyewahi kuwa Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Mary Mwanjelwa ameibukia kwenye kampeni za uchaguzi mdogo wa ubunge Mbarali zinazoendelea.

Dk. Mwanjelwa aliibuka juzi kwenye kampeni za kumnadi mgombea ubunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Bahati Ndingo ambapo alishiriki kwenye kampeni katika Kata ya Mwatenga.

Aliwaomba wananchi wa Mbarali wamchague Bahati akisema kuwa ni mgombea sahihi ambaye atasaidia kuwasilisha kero zao serikalini na kuzitafutia ufumbuzi.

Alisema kabla ya kuanza kuwania nafasi hiyo, Bahati alikuwa Mbunge wa Viti Maalumu kupitia Jumuiya ya Wazazi Taifa na alikuwa anawatetea wananchi wa jimbo hilo.

Kwa upande wake Bahati alisema endapo wananchi wa jimbo hilo watamchagua atahakikisha anashirikiana na viongozi wengine wa chama na serikali katika wilaya hiyo kutatua kero mbalimbali zinazowakabili.

Alisema tatizo kubwa la Mbarali ni migogoro kati ya wananchi na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ambayo imekuwa ikisababishwa na upanuzi wa mpaka wa hifadhi hiyo kupitia Tangazo la Serikali Namba 28 (GN.28) la Mwaka 2008.

Alisema wananchi wamekuwa wakikosa maeneo ya kufanyia shughuli zao za uzalishaji kutokana na maeneo yao mengi kuchukuliwa na kuwa sehemu ya hifadhi.

"Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ni msikivu sana, tuliomba turejeshewe baadhi ya maeneo akakubali na kuturejeshea hekta 74,000 naamini tukiendelea kuomba tunaweza tukapata maeneo mengi zaidi," alisema Bahati.

Alisema wananchi wa Mbarali wamekuwa wakifanya kazi kwa bidii hasa kwenye shughuli za kilimo na hivyo wanahitaji mtu ambaye atawawakilisha vyema bungeni.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbarali, Mary Mbwilo alisema wagombea waliokuwa wameomba nafasi hiyo kwenye kura za maoni walikuwa zaidi ya 20 lakini Bahati akaonekana anafaa zaidi na ndipo chama kikamteua.

Alisema chama hicho kitapambana ili kuhakikisha kinapata ushindi na kutetea jimbo hilo ambalo kwa muda mrefu limekuwa ni ngome ya CCM.

Aliwataka wananchi wa jimbo hilo kutorubuniwa na wagombea wa vyama vingine vya upinzani ambao alidai kuwa wamekuwa wakiwapotosha wananchi.

Uchaguzi katika jimbo hilo unatarajiwa kufanyika Septemba 19 mwaka huu ili kuziba pengo la Francis Mtega ambaye alifariki.



# Dk. Mwinyi: TIRA imeleta mafanikio makubwa Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, (pichani chini) amesema kwa miaka mingi Serikali ya Zanzibar ilikuwa ikikata bima nje ya nchi, lakini kwa sasa Mamlaka ya Bima Tanzania (TIRA) imeleta mafanikio makubwa kwa kuokoa fedha nyingi.

Aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar wakati akizungumza na uongozi wa TIRA waliofika kwa lengo la kuwatambulisha mabalozi wapya wa kuitangaza taasisi hiyo. Pamoja na mambo mengine, Dk. Mwinyi aliwapongeza mabalozi wapya walioteuliwa na TIRA kuendelea kuitangaza taasisi hiyo kwa viongozi wa umma wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mabalozi hao ni Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Mhandisi Zena Ahmeid Saidi, Wanu Hafidh Ameir na Japhet Hasunga wote ni wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Naye, Kamishna wa Bima, Dk. Baghayo Saqware, kwenye mazungumzo hayo alisema mafaniko yaliyopatikana na TIRA kwenye sekta ya bima ikiwemo ongezeko la asilimia 1.68 kwenye pato la taifa kwa mwaka 2021 kutoka asilimia 0.56 kwa mwaka 2020.

Alisema taasisi hiyo imeendelea kuongeza gawio kwa serikali kutoka Julai 2022 hadi Juni 2023 kwa kutoa Sh. bilioni 2.9. Akizungumzia kuhusu mafanikio kwenye sekta ya ajira, Kamishna Saqware alisema hadi Septemba 2022, TIRA ilitoa ajira za kudumu kwa Watanzania 4,173 ikilinganishwa na 3,208 kipindi kama hicho mwaka 2021.

Mabalozi hao wa TIRA, waliteuliwa Februari mwaka huu, wakikabidhiwa majukumu ya kutoa ushauri kwa mamlaka na sekta ya bima kuhusu maendeleo ya sekta hiyo.

Jukumu lingine ni kutoa elimu kwa umma juu ya masuala ya bima katika ngazi mbalimbali ikiwemo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi, makatibu wakuu wa Tanzania Bara na Visiwani, mashirika ya umma na taasisi nyingine.

Tangu kuteuliwa kwa mabalozi hao tayari wamepewa mafunzo ya kuwajengea uwezo kuhusu umuhimu wa bima, kutoa elimu kwa umma.



# Nice One Beach yafungwa tuhuma kujihusisha na ukahaba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, ameifungia baa ya Nice One Beach iliyopo Mangapwani kutokana na kukiuka taratibu za biashara na kujihusisha na biashara ya ukahaba.

Uamuzi huo umefanyika baada ya mkuu huyo wa mkoa kupokea malalamiko kutoka kwa wanakijiji wa Bubwini na Mangapwani ya kwamba baa hiyo imekuwa kero kwao kutokana na kujihusisha na vitendo vya ukahaba ambavyo ni kinyume na maadili.

Licha ya kupokea malalamiko hayo, Ayoub alifanya ziara ya kushtukiza katika baa hiyo na kujiridhisha kuwapo kwa tuhuma hizo.

Alisema ni kweli nchi inahitaji utalii wa ndani na nje lakini haijawahi kutangaza kuwa inahitaji madanguro na ukahaba.

"Hata leseni yenu ya kamisheni ya utalii naisitisha nitaiagiza kamisheni ya utalii waje wafanye mapitio mara moja kuhusu suala lenu la kulaza wageni katika eneo hili. Hapa nina mashaka makubwa, nafunga kila kitu sio baa, hoteli na muziki mpaka nitakapojiridhisha kama kweli zinakidhi haja na matakwa ya sheria zetu"alisema.

Awali akipokea malalamiko mbalimbali ya wananchi wa vijiji hivyo, walisema kuwa baa hiyo inakiuka mila na desturi za Wazanzibar na kusababisha vijana wa vijiji hivyo kujihusisha katika biashara ya ngono.

Mmoja wa mwanakijiji hicho, Mohammes Khamis, alisema "Vijana wetu wamebadilika wanajihusisha na vitendo viovu kwa sababu baa hiyo inajihusisha na vitendo viovu ikiwemo vya ukahaba, tumechoshwa na tabia hizi". Mmiliki wa baa hiyo, Ali Salum Ali, akizungumza kwa njia ya simu alikana kuwapo kwa tuhuma hizo katika baa yake.


## UNAUDITED RESULTS FOR THE QUARTER ENDED 30 JUNE 2023

SIMBA CEMENT
STRENGTH WITHIN

**Introduction**

**Dear Shareholders,**

We hereby present the unaudited annual results of Tanga Cement Public Limited Company (''Tanga Cement'' or the ''Company'') and its subsidiary (together, the ''Group'') for the quarter ended 30th June 2023.

Amidst the escalating competitive dynamics prevalent in the industry, the inadequate electricity provisioning, and the scarcity of hard currencies, mainly USD and EUR, in the forex market, the operational performance of the group has exhibited a favourable enhancement compared to the corresponding period in the preceding year's second quarter. The group navigated through marketing and operational impediments stemming from recurrent power disruptions and an atypical season of heavy rainfall, both of which carried the potential to adversely influence the group's financial metrics during the quarter. The subsequent Financial and Operational Overview segment provides a comprehensive elaboration of the group's performance.

We affirm our commitment to all stakeholders through our high-quality cement and clinker, and our contribution towards the sustainable growth and development of Tanzania, a demonstration of our brand – **"Strength Within"**.

The company has deployed the highest standards of health and safety protocols across all its operations and continues to enforce safety at the workplace to protect our employees and contractors.

**Macro-economic Overview**
The Group's growth outlook continues to be anchored in the growth in cement demand of the Tanzanian construction industry. The forecasted average annual headline inflation rate decreased to 3.6% in the second quarter of 2023 from 4.7% in reported in March 2023.

Economic performance during the year has improved with annual GDP growth of 5.7% in 2023 compared to 5.2% in 2022 (as published by Fitch Solutions). Whilst the increase in GDP was pleasing, the primary drivers for business performance remained the robust infrastructure investment and a strengthening consumer base. Government's actions to support the medium-term monetary policy inflation target of 5% also supported demand for our products.

The Group remains optimistic of the positive impact of infrastructure development plans under the Government's Development Vision 2025 programme and expect the projects to continue gaining momentum in 2023. The Group is confident with the initiatives that the Government has taken to combat the effects of increase in oil prices as well as the impact of the scarcity of major foreign currencies and commits to working together with the Government in growing the economy.

**Financial and Operational Overview**
The company experienced a marginal decline of 5% in sales revenue, reaching TZS 55 billion in comparison to the TZS 58.3 billion achieved during the second quarter of 2022. Gross profit witnessed a substantial increase of 25% to TZS 14.1 billion, surpassing the TZS 11.2 billion attained in the corresponding period of the previous year. This growth was supported by the gross margin of 25%, which was a significant improvement from the 19% recorded in the first quarter of 2022. This upward trajectory is attributed primarily to the diligent implementation of cost containment strategies in our operations, in line with the company's drive for enhanced efficiency..

EBITDA exhibited a remarkable surge of 63%, reaching TZS 9.3 billion compared to the previous year's TZS 5.7 billion in the second quarter of 2022. This substantial improvement can be attributed to the intentional implementation of cost containment strategies by the management team. Despite challenges such as power outages and fluctuations leading to elevated maintenance expenses, which management successfully navigated to effectively control both maintenance and administrative costs.

The Group reported a loss before tax of TZS 2.1 billion in Q2, 2023, showcasing an improvement from the prior year's loss before tax of TZS 2.4 billion in 2022. This decline in pre-tax loss can be primarily attributed to the impressive performance highlighted in the aforementioned metrics, specifically the gross profit and EBITDA.

Cash generated from trading activities increased by 438% from TZS 1.7bn recorded in June 2022 to TZS 9bn in June 2023. Net cash flows from operations increased by 558% from TZS 1.4bn recorded in June 2022 to TZS 9bn in June 2023.This increase was attributed to an improvement in the gross margin and EBITDA of 6% and 63% respectively as a result of management's adept execution of cost management and cashflow enhancement strategies.

The Group continues to be committed to its sales, logistics and cost optimisation initiatives as it continually seeks to enhance value for its stakeholders. The Group maintains its positive outlook for 2023 despite the very competitive landscape and the economic impact of global geopolitical unrest. Government initiatives to spur on economic growth through infrastructure development and promotion of local industries is expected to boost local cement output and consumption while curbing the influx of cheap imported cement.

**Dividend**
The company did not declare an interim dividend to shareholders in 2023 to remain prudent with available cash resources in order to remain sustainable through the global economic uncertainties and the high fuel prices coupled with pronounced scarcity of major foreign currencies affecting the local economy. The board has decided to continue committing available current cash generated to the operational commitments. The Board will evaluate the financial performance throughout the 2023 financial year when considering any further dividend declarations.

**Proposed acquisition by Scancem International DA**
Shareholders are reminded of the announcement regarding the proposed acquisition by Scancem International DA of 68.33% of the shares in Tanga Cement PLC from Afrisam Mauritius Investment Holdings Limited on 27 October 2021 and the most recent update on the transaction issued by the Company on 24 April 2023.

**Conclusion**
Tanga Cement remains grateful to its staff for their passion and dedication to the company, and to its customers for their belief in the Simba Cement brand, as the company works to achieve its short- and long-term growth strategy.

With Tanzania remaining a significant player in the East African construction market, cement output is anticipated to increase and Tanga Cement is well positioned to take advantage of the growth opportunities in the regional market.

For and on behalf of the Board

**Patrick Rutabanzibwa**
Chairman of the Board

| **Consolidated and separate statements of profit or loss and other comprehensive income** FOR THE PERIOD ENDED 30 JUNE 2023 | Group Jun-23 TZS'000 | Group Jun-22 TZS'000 | Company Jun-23 TZS'000 | Company Jun-22 TZS'000 |
|---|---|---|---|---|
| Revenue from contracts with customers | 55,030,505 | 58,229,918 | 55,030,505 | 58,229,918 |
| Cost of sales | (40,950,893) | (46,998,234) | (40,950,892) | (46,998,234) |
| **Gross profit** | **14,079,612** | **11,231,684** | **14,079,613** | **11,231,684** |
| Other income | 49,965 | 588,793 | 47,863 | 586,693 |
| Other expenses | - | - | - | - |
| Selling expenses | (843,964) | (781,605) | (843,964) | (781,605) |
| Administration expenses | (4,214,232) | (5,368,956) | (4,389,324) | (5,366,789) |
| Depreciation charge | (4,852,768) | (4,754,486) | (4,870,088) | (4,764,205) |
| Impairment and other charges | 10,224 | - | 10,224 | - |
| Decrease/ (increase) in expected credit losses | 224,779 | 53,665 | (26,101) | (1,834) |
| **Operating profit** | **4,453,616** | **969,095** | **4,008,223** | **903,944** |
| Interest expense | (6,341,771) | (3,930,427) | (6,344,028) | (3,931,821) |
| Finance income | 10,774 | 48 | 10,774 | 48 |
| Foreign exchange and fair value (losses)/gains | (242,244) | 520,920 | (251,409) | 518,958 |
| **Loss before tax** | **(2,119,625)** | **(2,440,364)** | **(2,576,440)** | **(2,508,871)** |
| Income tax (charge)/credit | (294,820) | 481,223 | (294,820) | 481,223 |
| **Loss for the period** | **(2,414,445)** | **(1,959,141)** | **(2,871,260)** | **(2,027,648)** |
| **Other comprehensive income** | | | | |
| **"Other comprehensive income to be reclassified to profit or loss in subsequent periods (net of tax):"** | | | | |
| Exchange differences on translation of foreign operations | - | - | - | - |
| **Other comprehensive income net of tax** | - | - | - | - |
| **Total comprehensive income for the year, net of tax** | **(2,414,445)** | **(1,959,141)** | **(2,871,260)** | **(2,027,648)** |
| **Loss for the year attributable to:** | | | | |
| Owners of the parent | (2,414,445) | (1,959,141) | (2,871,261) | 2,027,648 |
| Non-controlling interests | - | - | - | - |
| | **(2,414,445)** | **(1,959,141)** | **(2,871,261)** | **2,027,648** |
| **Total comprehensive income for the year attributable to:** | | | | |
| Owners of the parent | (2,414,445) | (1,959,141) | (2,871,261) | (2,027,648) |
| Non-controlling interests | - | - | | |
| | **(2,414,445)** | **(1,959,141)** | **(2,871,261)** | **(2,027,648)** |
| | **Jun 23 TZS/share** | **Jun 22 TZS/share** | | |
| Basic and diluted loss per share | **(38)** | **(31)** | | |

| **Consolidated and separate statements of financial position** AS AT 30 JUNE 2023 | Group Jun-23 TZS'000 | Group Jun-22 TZS'000 | Company Jun-23 TZS'000 | Company Jun-22 TZS'000 |
|---|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | | |
| **Non-current assets** | | | | |
| Property, plant and equipment | 281,560,529 | 293,680,789 | 280,828,827 | 292,871,613 |
| Right-of-use assets | 4,618,068 | 4,911,950 | 4,616,876 | 4,862,445 |
| Investment property | 503,664 | 549,120 | - | - |
| Investment in subsidiary | - | - | 420,995 | 552,564 |
| Financial asset - Interest rate cap | 7,864,730 | 4,643,018 | 7,864,730 | 4,643,018 |
| Deferred tax asset | - | 38,307 | - | 38,307 |
| | **294,546,991** | **303,823,184** | **293,731,428** | **302,967,947** |
| **Current assets** | | | | |
| Due from employees' share trust | - | - | 773,467 | 773,467 |
| Inventories | 87,781,303 | 74,067,338 | 87,781,303 | 74,067,338 |
| Trade and other receivables | 4,973,101 | 11,573,978 | 5,151,031 | 11,553,878 |
| Current income tax recoverable | 8,689,931 | 6,232,000 | 8,186,454 | 6,232,000 |
| Cash and bank balances | 8,532,201 | 10,223,228 | 8,453,994 | 9,440,308 |
| | **109,976,536** | **102,096,544** | **110,346,249** | **102,066,991** |
| Non-current assets held-for-sale | - | 3,870 | - | - |
| **TOTAL ASSETS** | **404,523,527** | **405,923,598** | **404,077,677** | **405,034,938** |
| **EQUITY AND LIABILITIES** | | | | |
| **Equity** | | | | |
| Issued capital | 1,273,421 | 1,273,421 | 1,273,421 | 1,273,421 |
| Translation reserve | - | (67,490) | - | - |
| Treasury shares | (773,466) | (773,466) | - | - |
| Retained earnings | 105,739,874 | 135,956,085 | 104,046,042 | 134,487,760 |
| **Equity attributable to owners of the parent** | **106,239,829** | **136,388,550** | **105,319,463** | **135,761,181** |
| Non-controlling interest | - | - | - | - |
| **Total equity** | **106,239,829** | **136,388,550** | **105,319,463** | **135,761,181** |
| **Non-current liabilities** | | | | |
| Lease liabilities | 4,508,395 | 4,533,294 | 4,412,199 | 4,433,728 |
| Provision for site restoration | 30,014 | 29,637 | 30,014 | 29,637 |
| Term borrowings: Non-current portion | 221,398,551 | 199,533,377 | 221,398,551 | 199,533,377 |
| Deferred tax liability | 950,784 | - | 950,784 | - |
| | **226,887,744** | **204,096,308** | **226,791,548** | **203,996,742** |
| **Current liabilities** | | | | |
| Lease liabilities | 673,668 | 655,638 | 659,294 | 767,518 |
| Trade and other payables | 43,084,354 | 37,653,438 | 43,308,995 | 37,019,388 |
| Contract liabilities | 8,636,370 | 8,019,035 | 8,996,815 | 8,379,480 |
| Bank overdrafts | 19,001,562 | 19,110,629 | 19,001,562 | 19,110,629 |
| | **71,395,954** | **65,438,740** | **71,966,666** | **65,277,015** |
| **Total liabilities** | **298,283,698** | **269,535,048** | **298,758,214** | **269,273,757** |
| **TOTAL EQUITY AND LIABILITIES** | **404,523,527** | **405,923,598** | **404,077,677** | **405,034,938** |

| **Consolidated and separate statements of cash flows** FOR THE PERIOD ENDED 30 JUNE 2023 | Group Jun-23 TZS'000 | Group Jun-22 TZS'000 | Company Jun-23 TZS'000 | Company Jun-22 TZS'000 |
|---|---|---|---|---|
| **OPERATING ACTIVITIES** | | | | |
| Cash generated from operating activities | 8,966,256 | 1,667,665 | 9,173,553 | 949,747 |
| Interest income received | 842,447 | 96 | 842,447 | 96 |
| Income taxes paid | (805,679) | (300,106) | (788,637) | (300,106) |
| **Net cash flows from operating activities** | **9,003,024** | **1,367,655** | **9,227,363** | **649,737** |
| **INVESTING ACTIVITIES** | | | | |
| Purchase of property, plant and equipment | (3,356,755) | (2,440,684) | (3,356,755) | (2,440,684) |
| **Net cash flows used in investing activities** | **(3,356,755)** | **(2,440,684)** | **(3,356,755)** | **(2,440,684)** |
| **FINANCING ACTIVITIES** | | | | |
| Principal repayments - lease liabilities | (155,536) | (318,066) | (155,536) | (318,066) |
| Lease liability interest paid | - | (4) | - | (4) |
| Interest paid - overdrafts | (949,050) | (814,212) | (949,050) | (814,212) |
| **Net cash flows used in financing activities** | **(1,104,586)** | **(1,132,282)** | **(1,104,586)** | **(1,132,282)** |
| **Net increase/(decrease) in cash and cash equivalents** | **4,541,683** | **(2,205,311)** | **4,766,022** | **(2,923,229)** |
| Net foreign exchange differences | (483,249) | 28,780 | (727,476) | 28,781 |
| Cash and cash equivalents at 1 January | (14,527,795) | (6,710,870) | (14,586,114) | (6,775,873) |
| **Cash and cash equivalents at end of period** | **(10,469,361)** | **(8,887,401)** | **(10,547,568)** | **(9,670,321)** |

**Information to Members**
The company secretary would like to inform the members that dividends can be directly transferred to their bank

Members can contact The Dar es Salaam Stock Exchange on +255 (0)22 2123983 or on +255 (0)22 2128522 for information on how to have the dividends deposited directly into their bank

**Patrick Rutabanzibwa**
Chairman
25 AUGUST 2023

**R Swart**
Managing Director

**Q Ganijee**
Company Secretary

**Tanga Cement Public Limited Company**
P O Box 5053
Tanga
Tanzania
info@simbacement.co.tz

SYSTEM CERTIFICATION ISO 9001 SGS

217587202

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**HALIMA S. MAGAGULA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0771-0015** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ASKOFU ADRIAN MKUBA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015 na cheti cha kidato cha nne private candidate chenye index namba **P2517-0207** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa **ALFA SECONDARY SCHOOL CENTRE** mwaka 2016. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA **PHQ/MOR/MVO/1293/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya BAGAMOYO**
**Kituo cha KEREGE Mkoa PWANI**

**Shauri la Ndoa Na....38......../2023**

**Jina la mdai................................ESTER MWAKATOBE NDENUKA**

**Jina la mdaiwa..................................ISMAIL EMMANUEL MSENGI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa ISMAIL EMMANUEL MSENGI**

**Kwa kuwa Mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake yao kwamba ( Eleza hapa habari za Madai)**
**KUJA KUJIBU MADAI YA TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 15 mwezi 09 mwaka 2023 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

**Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 4 mwezi 9 mwaka 2023**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 27 OF 2023**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**

**BY JANE FRANK MDOE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **04th day of October 2023**

Dated at Korogwe this **4th day of September 2023**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BARTHOLOMEO LUCAS FISSOO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 670 AEL** aina ya **TOYOTA LAND CRUISER.** Chassis namba **HZJ75RV00226612.** Engine namba **IHZ0157953.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/MON/1415/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FRANCIS GASPER LUMEYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **TVS KING** yenye usajili namba **MC390BKM** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/1433/2023**

## MNADA WA HADHARA

Kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa sugu. Mnada utaendeshwa na madalali tajwa hapo chini kwa idhini ya **Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd** kama ilivyotangazwa gazetini:-

| Mdhamini/ Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada/ Dalali |
|---|---|---|
| Bernard Daud Nkeyemba | Nyumba- Madale DSM | 11. 09.2023 (**Marudio**) DENNESTO CO. LTD |
| Gregory Isdory Wenceslaus | Plot – Kimara-King'ong'o -DSM **Plot- Kibamba Mkuranga** | 15.09.2023 (**Marudio**) White miracles **12.09.2023** |
| Yahaya Khalid Ally | Nyumba- Kihonda Morogoro | 22.09.2023 (**Marudio**) Diamond Credit |
| Bakari Fakhi bakari | Nyumba- iliyopo Kinyamwezi-DSM | SEPCO Debt Collector 06.10.2023 |
| Hamida Mohamed Aley | Plot- Tandika (Mtaa Nyambwera) | RAPITECH Solutions Ltd – 26.09.2023 |
| Jerome Jerome Tesha | Plot – Mkuranga (Utungemwago) | RAPITECH Solutions Ltd – 28.09.2023 |
| Biswaro Zebedayo Msase | Nyumba (Kwembe) Mloganzila-DSM | RAISSA CO. LTD 29.09.2023 (**Marudio**) |
| Ridhiwan Khutuba Kyela/ Jonathan Shirima | Nyumba- ipo Kibondemaji Mbagala | GEMSUD Investment Ltd – 27.09.2023 |
| Hilda Archady Kikatuka | Nyumba - Mbugani Kishiri Mwanza | Mase International Ltd 21.09.2023 |

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**LUKUNGU INVESTMENT COMPANY LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 980 DKW.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/IRI/IRI/427/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BONY PETER IROGA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 211 BUV** aina ya **MITSUBISHI CANTER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **TAR/RB/1139/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EMMANUEL MARCEL KILANGI** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 209 EAB** aina ya **TOYOTA PRIMIO** yenye **CHASSIS NO.NZT2405023467.** ENGINE NO.**INZB159657.** Yeyote atayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi **PHQ/MWA/ILE/1213/2023.**

## KUPOTEA KADI YA BAJAJI

**RAHEL HINDA BWISU** anatangaza kupotelewa na Kadi ya Bajaji aina **TVS** yenye namba za usajili **MC 281 CKH.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Rahel Hinda Bwisu kwa simu namba **0719651044** TAARIFA YA POLISI: **MAS/RB/910/2022.**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM,MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KITAIFA/KIMATAIFA

# Usiri watawala kiongozi wa Korea Kaskazini, Putin wakikutana

**New York,** MAREKANI

KIONGOZI wa Korea Kaskazini, Kim Jong Un anapanga kusafiri hadi Russia mwezi huu kukutana na Rais Vladimir Putin, imeelezwa.

Mahali halisi patakapofanyika mkutano uliopangwa haijulikani. Hakukuwa na maoni yaliyotolewa mara moja kuhusu ripoti hiyo, ambayo pia iliangaziwa na vyombo vingine vya habari vya Marekani kutoka Korea Kaskazini au Russia.

Viongozi hao wawili watajadili uwezekano wa Korea Kaskazini kuipatia Moscow silaha za kusaidia vita vyake nchini Ukraine, Ofisa wa Kimarekani alidokeza.

Vyanzo vya habari vililiambia gazeti la New York Times kwamba Kim ana uwezekano mkubwa wa kusafiri kwa treni ya kivita.

Mkutano huo wenye uwezekano wa kufanyika unawadia baada ya Ikulu ya White House, kusema kwamba ina habari mpya kuhusu mazungumzo ya silaha kati ya nchi hizo mbili yanaendelea.

Msemaji wa Baraza la Usalama la Kitaifa, John Kirby alisema Waziri wa Ulinzi wa Russia, Sergei Shoigu, alijaribu kuishawishi Pyongyang kuiuzia Russia risasi za kivita, wakati wa ziara ya hivi majuzi nchini Korea Kaskazini.

Silaha zinazotarajiwa kuzungumziwa ni pamoja na kombora la masafa marefu la Hwasong, linaloaminika kuwa la kwanza la ICBM nchini humo kutumia fueli ngumu, Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Kim kufungua milango ya nchi kwa wageni wa kigeni tangu janga la Uviko-19.

Julai, mwaka huu, Waziri wa Ulinzi wa Russia, Shoigu alitembelea Korea Kaskazini.

Putin na Kim tangu wakati huo wamebadilishana barua na kuahidi kuongeza ushirikiano wao wa pande mbili

Kuna wasi wasi huko Washington na Seoul juu ya kile ambacho Korea Kaskazini itapata kwa makubaliano kama hayo, ambayo yanaweza kusababisha kuongezeka kwa ushirikiano wa kijeshi kati ya nchi hizo mbili za Asia.

Siku ya Jumatatu, idara ya ujasusi ya Korea Kusini iliarifu kwamba Shoigu alipendekeza Russia, China na Korea Kaskazini zifanye mazoezi ya pamoja ya wanamaji, sawa na yale yaliyofanywa na Marekani, Korea Kusini na Japan.

Hofu nyingine ni kwamba Urusi inaweza kuipatia Korea Kaskazini silaha katika siku zijazo, wakati ambapo Pyongyang inazihitaji zaidi.

Hata hivyo, mpango huo unaweza kuishia kuwa wenye shughuli nyingi zaidi kuliko wa kimkakati. Kwa sasa, Russia inahitaji silaha na Korea Kaskazini iliyowekewa vikwazo na yenye kukabiliana na baa la njaa, inahitaji pesa na chakula.

Gazeti la New York Times liliripoti kwamba mkutano unaweza kufanyika katika mji wa bandari wa Vladivostok, kwenye pwani ya mashariki ya Russia.

**BBC**




Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya mbolea ya Yara Tanzania, Winstone Odhiambo, akizungumza wa washiriki wa Mkutano wa Kimataifa wa Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF), alipotembelea banda la kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

### KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

# Mshtakiwa ang'aka kizimbani Mkuu Upelelezi kumwita 'mhalifu mzoefu'

**Na Grace Gurisha**

REVOCATUS Muyela, mshtakiwa wa pili katika kesi ya mauaji ya Aneth Msuya, amemtaka Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Arusha, SSP David Mhanaya, kuacha kumchafua kwa kumwita mhalifu mzoefu.

Mshtakiwa mwingine katika kesi hiyo ya mwaka 2018, ni mke wa aliyekuwa mfanyabiashara maarufu, marehemu Erasto Msuya 'Bilionea Msuya'. Washtakiwa wote ni wakazi wa Arusha.

Muyela alitoa kauli hiyo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, wakati SSP Mhanaya akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Paul Kimweri, katika maswali ya kizimbani.

Shahidi huyo alifikia hatua hiyo baada ya Wakili Kimweri kumtaka aeleze tofauti ya majina ya mshtakiwa, yaani Revocatus Muyela, Revocatus Mollel na Revocatus Everest. P. Mollel.

Alidai kuwa alipokwenda kufanya upekuzi kwa hati ya dharura nyumbani kwa mshtakiwa namba mbili (Revocatus), alikuta cheti cha kuhitimu Mafunzo ya Mgambo chenye jina la Revocatus Mollel na kitabu cha miliki ya bastola chenye jina la Revocatus Everest. P. Mollel.

"Mtuhumiwa hakukataa haya majina kuyatumia, kwa sababu alisaini hati hii ya upekuzi pamoja na mashahidi huru. Kimsingi, hizi ndizo tabia za wahalifu wazoefu kutumia majina tofauti tofauti," alidai SSP Mhanaya.



Aneth Msuya



Bilionea Msuya

Baada ya SSP Mhanaya kutamka maneno hayo, mshtakiwa Revocatus alianza kuzungumza kwa sauti ya chini huku akionesha hisia za kuchukizwa na matamshi hayo.

Katika hali hiyo, Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, alisimama na kupinga kilichosemwa na shahidi.

**Kibatala:** Kauli ya shahidi inakinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na pia shahidi anakuwa anamhukumu mtuhumiwa.

**Kimweri:** Mheshimiwa Jaji, sioni jambo geni hapa ambalo shahidi amelizungumza, kwa sababu tangu juzi alikuwa analisema hili.

Wakati Kimweri anadai hayo, mshtakiwa Revocatus alitoa sauti akidai shahidi anamchafua kwa kumwita 'yeye mhalifu mzoefu wakati hamjui'.

"Ananijua mimi huyu? Hapa kuna waandishi wa habari, halafu anasema maneno haya! Huku ni kunichafua, kwa sababu hanijui kabisa!" mshtakiwa Revocatus alidai.

**Kibatala:** Ray (akimaanisha Revocatus), hebu nyamaza, acha kuzungumza. Shahidi atueleze kama kuna mahakama yoyote ilishamtia hatiani mtuhumiwa?

**Jaji:** (akaingilia) Bado sijaona mnachobishiania hapa katika haya majina.

**Kimweri:** Mimi sijaona tabu kwa anachokizungumza.

**Kibatala:** Mheshimiwa Jaji, iingie kwenye rekodi za mahakama kwamba haya ni maoni ya shahidi. Pia, shahidi huyo alidai kuwa simu za mshtakiwa wa kwanza, Mrita zilifanyiwa uchunguzi, lakini hazikuwa na uhusiano na tukio la mauaji ya Aneth, ambapo yeye alitumia simu zingine ambazo watakuja kuzielezea wataalamu.

Baada ya hoja ya Wakili Kibatala, SSP Mhanaya aliendelea kujibu maswali ya ufafanuzi kwamba, alimhoji mume wa marehemu Aneth, Wilbert Kimaro, lakini hawakubaini kama walikuwa na ugomvi, hasa katika tukio hilo la mauaji.

Pia, alidai kuwa Ripoti ya Awali ya Siri ya Jeshi la Polisi (First Crime Report) inaonesha watuhumiwa waliokamatwa awali, yaani Getruda Mfuru, Sabri Haji, Kimaro, Twaha Almasi na Amiri Saidi, walikamatwa Mei 25, 2016. Ripoti yenyewe iliandaliwa Julai 11, 2016.

"Kwa mujibu wa hii nakala, ninaona iliandaliwa 'kimagumashi', kwa sababu hizi ripoti zinaandaliwa palepale tukio linapotokea kutoka kwa Mkuu wa Upelelezi Wilaya, mkoa na kisha kwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai".

"Ukitaka kujua taarifa hii ni ya awali kwenye 'brief of particular', inaelekeza kuwa marehemu Aneth ambaye alikuwa ni mfanyakazi wa Wizara ya Fedha na Mipango, alikatwa shingo na watu wasiojulikana," alidai SSP Mhanaya.

Kwa upande wake, shahidi namba 23, Sajenti Mwaka, alieleza mahakamani jinsi alivyopokea vielelezo katika Kituo cha Polisi Kigamboni na kuvihifadhi. Vielelezo hivyo ni bahasha tatu zilizoandikwa kuwa kielelezo A (kisu), B (nguo ya ndani) na C (filimbi).

Alidai kuwa vielelezo hivyo alikabidhiwa na Afande John Benard. Aliingiza katika kitabu kinachohusiana na vielelezo hadi Agosti 28, 2016 asubuhi vilipochukuliwa tena na Afande Benard.

Kesi inaendelea kusikilizwa leo kwa upande wa mashahidi wa Upande wa Mashtaka.

Miriam ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya tuhuma za mauaji ya wifi yake, Aneth, aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake Kibada, Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa kukiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo.

# KMKM, JKU kivumbi Ngao ya Jamii J'mosi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MCHEZO wa Ngao ya Jamii wa kufungua rasmi pazia la Ligi Kuu ya Zanzibar msimu huu wa 2023/2024, umepangwa kuchezwa Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Mau Kisiwani Unguja.

Mchezo huo utaikutanisha miamba miwili ya soka visiwani hapa, Bingwa Mtetezi wa Ligi Kuu Zanzibar, 'Wanamaji' KMKM dhidi ya Mshindi wa Kombe la FA, Maafande wa JKU.

Akizungumza na gazeti hili jana, Afisa Habari wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Mohamed Kabwanga, alisema kwa msimu huu mchezo huo utapambwa na burudani tofautisha na michezo iliyopita.

Alisema kupitia mchezo huo pia ZFF imeandaa mpango maalum kwa ajili ya kutoa hamasa kwa mashabiki wa soka ili kufuatilia kwa karibu Ligi Kuu Zanzibar ambayo itaanza kutimua vumbi Septemba 13, mwaka huu.

Kabwanga alisema bado ZFF inaendelea na jitihada za kusaka wadhamini na kwamba wapo katika mazungumzo na kampuni mbalimbali lengo likiwa ni kuhakikisha wanapatikana mdhamini wa mchezo huo wa Ngao ya Jamii.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| KIJITONYAMA | NEZAK INVESTMENT LTD | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1019002 KIWANJA NAMBA P23439 KIFURU-KINYEREZI 2.NYUMBA YENYE HATI NA. 67242 KIWANJA NA. '637', KITALU 'F' BUHONGWA MWANZA 3..NYUMBA YENYE HATI NA. 70437 KIWANJA NA. '213', KITALU '14' BUNJU KINONDONI | 1. ZACHARIA ANTHONY KAPAMA 2. MARIANA ZACHARIAS BUKWIMBA 3.DAFROSA ATHONY KAPAMA | 1.KIFURU KINYEREZI-ILALA 2.BUHONGWA MWANZA 3.BUNJU KINONDONI | 15/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | MAMU PHARMACY | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.151,KITALU 'Q10' HATI NAMBA 143195-KIBAMBA | AHMAD KASSIM OMARY | KIBAMBA | 15/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | VICTOR STEVEN MANG'ANA | NYUMBA | VICTOR STEVEN MANG'ANA | UKONGA | 14/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | ROBERT CHACHA NYAMBARI | NYUMBA | ROBERT CHACHA NYAMBARI | KITUNDA MTAA WA KINYANTIRA | 19/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | PAULO GIRIMBE RAWE | NYUMBA | PAULO GIRIMBE RAWE | KIVULE-ILALA | 14/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | INNOCENT DIDAS MUMBURI | NYUMBA | KHADIJA SEIF SINKAMBA | VINGUNGUTI- ILALA | 20/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | JUTIA ABDALA SANZE | NYUMBA | JUTIA ABDALLA SANZE | PUGU BOMBANI -ILALA | 20/09/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | GADNER HATWABY DIBIBI | NYUMBA | ZUWEJA SELEMANI KAZEMBE | CHARAMBE-NZASA "A" | 21/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | KITETE-MBEYA | 11/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 17/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA ZENYE HATI YA MAUZIANO | FRENK SAMSON LEMAU | SHEWA-MBEYA | 20/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 11/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | MWANJELWA , MBEYA MJINI | 13/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | EMANUEL MOYO MASETA | 1.NYUMBA (3) 2.KIWANJA | EMANUEL MOYO MASETA | 1.IFWEKENYE -MBOZI 2.SONGWE | 15/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | JOSEPH RASHIDY MKONJA | NYUMBA | OLIVA YUSUPH MGENI | MBALIZI | 12/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | NDIMBWELU BANDEKISYE KAFWENDA | NYUMBA | PAULO KALOTA NDAWILA | NZOVWE-MBEYA | 13/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | IPYANA TIGER JUNIOR | NYUMBA | IPYANA TIGER JUNIOR | ILEMI-MBEYA | 14/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BARAKA PAUL DABAVUNJE | MBEYA | BARAKA PAUL DABAVUNJE | UYOLE | 20/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BRAITON REBEN MWANKEMWA | NYUMBA | BRAITON REBEN MWANKEMWA | IVUMWE | 19/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | SABAS PAUL MSELLE | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | SABAS PAUL MSELLE | SHIRIMATUNDA-MOSHI | 20/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | INTERCITY BUILDERS LIMITED | 1.DOLL 3DSAK42 TRAILER NO. T984 DAH 2. SDLG ROAD ROLLER NO. T423 DBV | INTERCITY BUILDERS LIMITED | KURASINI -DAR ES SALAAM | 20/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | SONGALELI SAMA MZEE | KIWANJA | SONGALELI SAMA MZEE | BUSWELU MWANZA | 12/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | GRACE ADONIAS MTEGO | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.22 KITALU 'N' HATI NA.4870 | BLASIUS SWAI KAGINA | BUNDA | 13/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | ABAS HAMAD ISSA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PETER NDULU MAHARAGE | MISUNGWI-MWANZA | 14/09/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JUMANNE MOHAMED KAPOLI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | MATHIAS CHARLES NDETTO | KISESA-MWANZA | 15/09/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARIA JOHN PETRO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JOHN PETRO KALISA | KILOLELI 'B' - MWANZA | 20/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.NYUMBA 2. KIWANJA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.IGELEGELE BUGARIKA 2. BUJINGWA-MWANZA | 19/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | OSCAR JOSSEY MUNIS | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | VERAELI ELIYA KOMBE | MWANANYAMALA -KINONDONI | 21/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 22/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MARIAM DARUWESHI IDDI | NYUMBA | MARIAM DARUWESHI IDDI | KIBUGUMO-KIGAMBONI | 14/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KINONDONI | VAM COMPANY LIMITED | NYUMBA | VENANT ANGELO BAKEMYA | BUNJU | 28/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | MTUMWA SALUM HAMAD | NYUMBA | MTUMWA SALUM HAMAD | PUGU-KINYAMWEZI | 20/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | RASHIDI SAIDI MSUYA | NYUMBA | RASHIDI SAIDI MSUYA | MBAGALA CHAMAZI | 21/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | HAMAD ABDALLAH MNEMBWE | NYUMBA | AHMAD ABDALLAH MNEMBWE | TANDALE-SOKONI | 21/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | BIZUNGU HARDWARE & GENERAL SUPPLIES | NYUMBA | HAWA JUMANNE SAID | MIPEKO MKURANGA | 24/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | AMANI OMARI NOMBWANI | NYUMBA | AMANI OMARI NOMBWANI | KIGOGO-KIGAMBONI | 26/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | MINIHAJI HUSSENI MSHALE | NYUMBA | MINIHAJI HUSSENI MSHALE | G/MBOTO ULONGONI | 28/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | PETER BENEDICT NJOKA | NYUMBA | PETER BENEDICT NJOKA | MKURANGA-MLAMLENI | 24/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | ARIEL JOHN MNGEREJA | NYUMBA | ARIEL JOHN MNGEREJA | ZINGIZIWA | 31/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | PADONI KIBAYU SIMON | NYUMBA | PADONI KIBAYU SIMON | MAJOE-VIWEGE | 26/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | ATUPELE LABAN MWAIJIBE | NYUMBA | DR.ATUPELE LABAN MWAIJIBE | KIPUNGUNI KIPAWA-ILALA | 23/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | HAMISI MESHACK NGINYANYI | NYUMBA | HAMISI MESHACK NGINYANYI | TABATA- LIWITI | 28/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | SALUM RAJABU MCHOMVU | NYUMBA | SALUM RAJABU MCHOMVU | MAJOJE | 29/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | LISTER BENEDICT CHIMYA | NYUMBA | LISTER BENEDICT CHIMYA | KIMARA KING'ONG'O | 30/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | MAIMUNA ISAYA KIRINDO | NYUMBA | MAIMUNA ISAYA KIRINDO | MBEZI KIBANDA CHA MKAA | 30/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | EDNA ISHENGOMA RWEMILINZI | NYUMBA | EDNA ISHENGOMA RWEMILINZI | TEGETA 'A' | 31/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | REHEMA SAID KATEULE | NYUMBA | REHEMA SAID | MBEZI MAKABE | 31/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | ANTHONY DOMINIC FERNANDES | PAGALE | ANTHONY DOMINIC FERNANDES | MAPINGA BAGAMOYO | 27/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | HP PLANNERS & EVENTS MANAGEMENT LTD | NYUMBA (2) | 1.JAMES NDASKOI NNKO 2.DAPHROSER ABEID HAMZA | 1.TEGETA 2.KIGAMBONI | 20/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja , Shamba au Gari ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0745707008/0759282344/0714939933/0765999000**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

217586701


# STARS YAIFUATA ALGERIA IKIHITAJI POINTI MOJA KUFUZU AFCON 2023

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha timu ya soka ya Tanzania, Taifa Stars, kinatarajiwa kuwasili leo nchini Algeria kutoka Tunisia kwa ajili ya mechi ya mwisho kesho ya kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), zitakazofanyika mwakani nchini Ivory Coast, huku serikali ikisema safari hii hakukuwa na kamati ya hamasa baada ya kupata ushauri yakinifu ili kutowatia presha wachezaji.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), Cliford Ndimbo, amesema kikosi hicho kilitarajia kuondoka leo kwenye mji wa Tabarka uliopo Kaskazini Magharibi mwa Tunisia ambapo kiliweka kambi kwenda kwenye mji wa Annaba uliopo Kaskazini mwa nchi ya Algeria ambako mchezo huo utachezwa kesho dhidi ya timu ya taifa hilo ambayo tayari imefuzu.

**"Kikosi kinaendelea vizuri na maandalizi kuelekea mechi ya marudiano ya kufuzu AFCON dhidi ya Algeria katika kambi inayoendelea hapa nchini Tunisia, kesho (leo), tunatarajia kuondoka kwenye mji huu wa Tabarka kwenda mji wa Annaba, Algeria ambako mechi yetu itachezwa, wachezaji wanaocheza soka la kulipwa nje wameshawasili nchini Algeria na tutaungana nao kesho (leo), ni Simon Msuva pekee kati yao ndiye tunaye hapa kambini," alisema Ndimbo.**

Alisema hali ya kikosi iko vizuri huku wakiwa na morali na kila mmoja anatamani mechi ifike wakiwa na nia ya dhati kuiona nchi yao ikitinga AFCON.

"Nia ya wachezaji, serikali, Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), benchi la ufundi na serikali ni kuhakikisha tunacheza fainali za AFCON kwa mara nyingine tena" alisema.

Naye Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma, (pichani chini) amebainisha kuwa safari hii hakukuwa na hamasa pamoja na kamati zake kama ilivyokuwa huko nyuma baada ya kupata ushauri.

"Matarajio yetu ni kufuzu ili kuweza kucheza fainali za Mataifa ya Afrika kule Ivory Coast mwakani, lakini hamasa kama unavyoona haijafanyika kama zile zilizofanyika kipindi kilichopita kwa sababu tulishauriwa sana hapa katikati, kwamba miongoni mwa mambo tunayokosea ni kuipa presha kubwa timu yetu, lakini yale ambayo serikali inatakiwa kuyafanya ndani ili kuhakikisha timu inakuwa kwenye kiwango kinachoridhisha na wachezaji wapo katika hali nzuri yote tumeyafanya huku ndani mpaka timu imesafiri na hata huko tunahakikisha ipo salama na huduma zote huku ikienda kwenye mchezo ikiwa katika nafasi ya kushinda," alisema.

Stars yenye pointi saba kwenye Kundi F, inahitaji ushindi au sare katika mechi itakayochezwa Uwanja wa 19 May, ili kuweza kufuzu bila kuangalia matokeo ya Niger dhidi ya Uganda ambazo zitacheza siku hiyo hiyo kwenye Uwanja wa Marrakech nchini Morocco.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### WAKOMAA NA SALAH

UJUMBE wa Saudi Arabia uko nchini England kufanya jaribio la mwisho la kuishawishi Liverpool kumuuza Mohamed Salah kwa pauni milioni 200 kabla ya Alhamisi, huku kukiwa na imani kwamba mshambuliaji huyo wa Misri mwenye umri wa miaka 31, yuko tayari kujiunga na Al-Ittihad. ***(Mail)***

### PEPE AKARIBIA BESIKTAS

KLABU ya Besiktas inakaribia kukamilisha dili la winga wa Arsenal na Ivory Coast, Nicolas Pepe mwenye umri wa miaka 28. ***(90 min)***

### ASHAURIWA ATOROKE

WINGA wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23, atajikuta nje ya kikosi cha Manchester United msimu huu kama hatapata njia ya kutorokea Saudi Arabia, amesema beki wa zamani wa klabu hiyo, Rio Ferdinand. ***(Telegraph)***

### RAMOS NA MAN UNITED

MLINZI wa zamani wa Hispania, Sergio Ramos, mwenye umri wa miaka 37, alikataa ofa ya mwisho ya kujiunga na Manchester United kabla ya kufikia mkataba wa kurejea Sevilla. ***(Sun)***

### ATAKIWA WEST HAM

KLABU ya West Ham inatarajiwa kuwasilisha dau la kumsajili kwa muda mfupi kiungo wa England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 30, wakati wa mapumziko ya michuano ya kimataifa. ***(Mail)***

### AWANIWA AL-ETTIFAQ

KLABU ya Al-Ettifaq inapania kumsajili winga wa Everton na Jamaica, Demarai Gray mwenye umri wa miaka 27, huku mchezaji huyo akitamani kuondoka Goodison Park. ***(Mail)***

### LASCELLES ANYATIWA

NAHODHA wa Newcastle United, Jamaal Lascelles mwenye umri wa miaka 29, ananyatiwa na Klabu ya Al-Shabab inayoshiriki Ligi ya Saudia. ***(Team Talk)***

### AKARIBIA ANDERLECHT

KLABU ya Anderlecht inakaribia kumsajili Kasper Schmeichel mwenye umri wa miaka 36, baada ya kuondoka Nice wiki iliyopita. Kipa huyo wa Denmark alizivutia Chelsea, Nottingham Forest na Brentford msimu wa majira ya joto. ***(Mail)***

### ERIC, DE BEEK KUUZWA

KLABU ya Manchester United bado inajaribu kuwauza beki wa Ivory Coast, Eric Bailly mwenye umri wa miaka 29 na kiungo wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek (26), huku kipindi cha usajili wa wachezaji katika Ligi ya Saudia kiendelea hadi kesho, Alhamisi. ***(Sun)***

### LLORIS KUBAKI SPURS

GOLIKIPA wa Tottenham Hotspur na Ufaransa, Hugo Lloris mwenye umri wa miaka 36, anatazamiwa kubaki katika klabu hiyo hadi angalau Januari baada ya kukataa ofa nyingi msimu wa majira ya joto. ***(Standard)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR: MIMI NA MESSI PALE PSG TUMEISHI KAMA KUZIMU

**JEDAH,** Saudi Arabia

**Yeye aliishi pande mbili za sarafu, alikwenda mbinguni na timu ya Argentina, lakini...**

MSHAMBULIAJI wa Brazil na Al Hilal, Neymar amesema "niliishi kuzimu" pamoja na mchezaji mwenzake wa zamani klabuni hapo, Lionel Messi walipokuwa pamoja pale Paris Saint-Germain.

**Wachezaji wote wawili waliondoka PSG msimu huu wa majira ya joto, huku Messi akijiunga na Inter Miami CF kama mchezaji huru na Neymar akihamia Klabu ya Al Hilal ya Saudia kwa uhamisho wa euro milioni 90.**

Alipoulizwa alijisikiaje kuhusu kumuona rafiki yake mkubwa Messi akinyanyua Kombe la Dunia akiwa na Argentina mwaka 2022, Neymar aliiambia Esporte Espetacular ya Globo katika mahojiano yaliyotolewa Jumapili: "Nilifurahi sana kwa mwaka aliokuwa nao.

"Kwa sababu aliishi pande zote mbili za sarafu. Alikwenda mbinguni na timu ya Argentina, akashinda kila kitu katika miaka ya hivi karibuni, na akiwa na Paris aliishi kuzimu, tuliishi kuzimu, yeye na mimi."

Messi na Neymar, ambao walikuwa wamecheza pamoja hapo awali Barcelona, walishinda mataji ya ligi wakiwa PSG, lakini walishindwa kuleta mafanikio ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa klabu hiyo.

Messi alipata ugumu kuzoea maisha kule Paris na alikiri mnamo Juni kwamba kulikuwa na "kuvunjwa moyo na kundi kubwa la mashabiki wa PSG" wakati wa misimu yake miwili katika klabu hiyo.

Wachezaji wote wawili walizomewa na kukejeliwa na mashabiki wa PSG kufuatia timu hiyo kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika kipindi cha miaka miwili iliyopita.

Messi, ambaye alifunga mabao 21 na kutengeneza mengine 20 katika michuano yote msimu uliopita, pia alilengwa na umati wa watu katika mchezo wake wa mwisho wa PSG wa nyumbani. Neymar alisema anaamini ukosoaji ambao yeye na Messi walifanyiwa haukuhitajika.

"Tunakasirika, kwa sababu hatupo bure, tupo kufanya bidii yetu, kuwa mabingwa, kujaribu kuweka historia," alisema Neymar, ambaye alikosa kipindi cha pili cha msimu uliopita kutokana na jeraha la kifundo cha mguu.

"Ndio maana tulianza kucheza pamoja tena, tulikuja pamoja huko ili tuweze kuweka historia. Kwa bahati mbaya, hatukufanikiwa."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 697,

MECHI KALI
LIBYA
VERSUS
EQUATORIAL GUINEA
1 | 3.17
X | 3.06
2 | 2.28

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA
MAOKOTO Deilee!
1. Ema Alphonce - 0654 109 XXX
2. Moza Mbwana - 0655 413 XXX
3. Jackson Biatusi - 0672 171 XXX
4. Mnahawa Mtikila - 0679 276 XXX
5. Omary Athumani - 0713 400 XXX
6. Jacqueline Elias - 0714 437 XXX
7. Ally Saidi - 0715 314 XXX
8. Zainabu Chubi - 0717 258 XXX
9. Christina Shangija - 0717 845 XXX
10. Esikar Mollel - 0719 320 XXX
20,000/=
KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GREALISH, ALEXANDER-ARNOLD WAJIONDOA KIKOSINI ENGLAND



**LONDON,** England

JACK Grealish na Trent Alexander-Arnold wamejiondoa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa cha England kitakachocheza mechi za kimataifa dhidi ya Ukraine na Scotland kutokana na kuwa majeruhi.

Wawili hao walitajwa miongoni mwa waliochaguliwa na kocha Gareth Southgate wakati 'Simba Watatu' hao wakiendelea na kampeni ya kufuzu kwa Euro 2024 dhidi ya Ukraine na kushiriki mechi ya kuadhimisha miaka 150 na Scotland mjini Glasgow.

Alexander-Arnold alitolewa dakika ya 71 wakati Liverpool ikishinda mabao 3-0 dhidi ya Aston Villa Jumapili, huku Grealish akikosa ushindi wa 5-1 wa Manchester City dhidi ya Fulham kutokana na jeraha la paja.

Taarifa kutoka kambi ya England imeeleza: "Jack Grealish na Trent Alexander-Arnold wameondolewa kwenye kikosi cha England kwa mechi za Septemba.

"Wawili hao waliripoti kwenye Uwanja wa St. George's Park Jumatatu, lakini wamejiondoa kwenye kikosi cha Simba Watatu baada ya uchunguzi wa majeraha waliyoyapata kabla ya kwenda kambini."

England hawana mpango wa kuwaita wachezaji wengine kwenye kikosi, ingawa Kieran Trippier atawasili leo Jumatano kwa sababu alichelewa kwa matatizo binafsi.

Alexander-Arnold atarejea Liverpool kwa matibabu na anatarajiwa kuwa nje ya uwanja kwa takriban wiki mbili, jambo linalomfanya kuwa na shaka katika safari ya Wolves baada ya mapumziko ya kimataifa.

Washambuliaji kama Phil Foden, James Maddison na Eberechi Eze watakuwa na matumaini ya kuanza bila Grealish, pamoja na Harry Kane na Bukayo Saka.

# Antony atemwa kwa tuhuma za unyanyasaj



**SAO PAULO,** Brazil

BRAZIL imemtema kikosini winga wa Manchester United, Antony baada ya madai ya unyanyasaji yaliyotolewa na mpenzi wake wa zamani.

Shirikisho la Soka la Brazil lilisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ameondolewa kwenye kikosi baada ya "mambo kujulikana" ambayo "yanahitaji kuchunguzwa".

Chombo cha habari cha Brazil, UOL, kilichapisha madai yaliyotolewa na mpenzi wa zamani wa Antony Jumatatu.

Polisi mjini Sao Paulo na Greater Manchester wanachunguza madai hayo, ambayo mchezaji huyo ameyakanusha.

"Ninaweza kusema kwa utulivu kwamba shutuma hizo ni za uongo na kwamba ushahidi uliotolewa tayari na ushahidi mwingine utakaotolewa unaonesha kwamba sina hatia kwa tuhuma hizo," alisema A[illegible] ony kupitia mitandao [illegible] kijamii.

"Nina imani kuwa uch[illegible] guzi unaoendelea wa p[illegible] utadhihirisha ukweli ku[illegible] su kutokuwa na hatia."

Antony anashutum[illegible] kwa kumshambulia mp[illegible] wake wa zamani, Gabr[illegible] Cavallin kwa kumpiga [illegible] kichwa kwenye chu[illegible] cha hoteli mjini Manc[illegible] ter mnamo Januari 15[illegible] kumwacha akiwa ameu[illegible] na alihitaji matibabu.

,654,550

JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.06/09/23 | 21:00 | Sonderjyske vs Vejle BK | 2.60 | 3.36 | 2.39 |
| 02.06/09/23 | 22:00 | Tigres FC (COL) vs Bogota FC | 2.27 | 2.76 | 3.37 |
| 03.06/09/23 | 22:00 | Real Soacha Cundinamarca vs Leones FC | 2.35 | 3.09 | 2.84 |
| 04.07/09/23 | 00:00 | Orsomarso vs Deportes Quindio | 3.10 | 2.95 | 2.28 |
| 05.07/09/23 | 00:30 | Jocoro FC vs Once Municipal | 2.38 | 3.22 | 2.71 |
| 06.07/09/23 | 03:00 | Memphis 901 FC vs Tampa Bay Rowdies | 2.90 | 3.25 | 2.24 |
| 07.07/09/23 | 21:45 | Wales vs South Korea | 2.50 | 3.31 | 2.79 |
| 08.08/09/23 | 20:30 | Niort vs Cholet | 2.45 | 3.15 | 2.79 |
| 09.08/09/23 | 20:30 | US Marignane vs Nancy | 2.85 | 3.16 | 2.40 |
| 10.08/09/23 | 21:45 | Luxembourg vs Iceland | 2.65 | 3.19 | 2.71 |
| 11.08/09/23 | 22:00 | Levante vs Espanyol | 2.31 | 3.02 | 3.07 |
| 12.08/09/23 | 22:00 | Saudi Arabia vs Costa Rica | 2.47 | 3.28 | 2.85 |
| 13.09/09/23 | 00:00 | Ituano SP vs Vila Nova GO | 2.66 | 2.76 | 2.76 |

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 06/09/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 10:00 | 1423 | Myanmar U23 vs Kyrgyzstan U23 | 6.51 | 4.02 | 1.43 |
| 11:30 | 5874 | India U23 vs Maldives U23 | 1.61 | 4.08 | 4.28 |
| 12:00 | 2565 | Singapore U23 vs Yemen U23 | 6.50 | 3.96 | 1.44 |
| 12:00 | 5244 | Syrian Arab Republic vs Malaysia | 1.66 | 3.81 | 5.09 |
| 13:00 | 4376 | Consadole Sapporo vs Yokohama F Marinos | 2.43 | 3.67 | 2.40 |
| 13:00 | 4513 | FC Tokyo vs Avispa Fukuoka | 2.04 | 3.15 | 3.41 |
| 13:00 | 4609 | Gamba Osaka vs Urawa Red Diamonds | 2.69 | 3.20 | 2.40 |
| 13:30 | 2424 | Nagoya Grampus vs Kashima Antlers | 2.37 | 3.00 | 2.90 |
| 15:00 | 1510 | Iran U23 vs Hong Kong U23 | 1.10 | 7.31 | 19.30 |
| 16:00 | 2441 | Red Arrows vs FC Muza | 1.74 | 3.13 | 4.65 |
| 16:00 | 2527 | Cambodia U23 vs Lebanon U23 | 11.17 | 5.28 | 1.22 |
| 16:30 | 5604 | Thailand U23 vs Philippines U23 | 1.11 | 6.52 | 21.41 |
| 17:30 | 5586 | Syria U23 vs Oman U23 | 2.10 | 3.21 | 3.21 |
| 17:45 | 3844 | Oman vs Palestine | 2.06 | 3.38 | 3.59 |
| 18:00 | 1388 | Loko Vltavin vs Dukla Prague | 10.19 | 6.12 | 1.19 |
| 18:00 | 1712 | Opava B vs MFK Havirov | 1.69 | 4.00 | 3.60 |
| 18:00 | 2037 | IF Lyseng vs Middelfart | 6.08 | 4.76 | 1.38 |
| 18:00 | 2281 | FC Hlinsko vs SK Lisen | 8.98 | 6.94 | 1.18 |
| 18:00 | 2433 | Fjordager IF vs Hvidovre IF | 28.48 | 11.19 | 1.03 |
| 18:00 | 3466 | SK Kladno vs Varnsdorf | 5.06 | 5.06 | 1.42 |
| 18:00 | 4261 | Ceska Lipa vs MFK Chrudim | 6.96 | 5.94 | 1.27 |
| 18:00 | 4361 | FK Spartak Sobeslav vs Hradec Kralove | 17.37 | 8.38 | 1.08 |
| 18:00 | 4464 | Dalum vs FC Fredericia | 20.37 | 9.37 | 1.06 |
| 18:00 | 4542 | SK Zapy vs Taborsko | 4.57 | 5.08 | 1.46 |
| 18:00 | 4689 | Viby IF vs VSK Arhus | 4.08 | 3.93 | 1.66 |
| 18:00 | 5363 | SK Petrin Plzen vs FC Viktoria Marianske Lazne | 2.75 | 3.76 | 2.13 |
| 18:30 | 5884 | Bahrain U23 vs Palestine U23 | 2.10 | 3.21 | 3.21 |
| 19:00 | 2926 | Ringkobing IF vs Kolding IF | 15.25 | 7.12 | 1.12 |
| 19:00 | 3376 | Wurzburg vs Regensburg II | 2.38 | 3.51 | 2.53 |
| 19:00 | 3403 | Georgia U21 vs Gibraltar U21 | 1.03 | 9.98 | 35.66 |
| 19:00 | 3486 | Hillerod vs Lyngby | 4.88 | 4.27 | 1.51 |
| 19:00 | 3920 | FC Neptunas Klaipeda vs FK Panevezys B | 1.39 | 4.54 | 5.85 |
| 20:00 | 2018 | SG Dynamo Schwerin vs Optik Rathenow | 2.15 | 3.67 | 2.75 |
| 20:00 | 2579 | AB Taarnby vs Nykobing FC | 5.28 | 4.16 | 1.49 |
| 20:30 | 2845 | Eintracht Norderstedt vs FC Teutonia 05 | 2.96 | 3.62 | 2.06 |
| 21:00 | 1273 | Sonderjyske vs Vejle BK | 2.40 | 3.36 | 2.59 |
| 21:00 | 1415 | Malta vs Gibraltar | 1.57 | 3.81 | 6.21 |
| 21:00 | 5502 | FC Arlanda vs Kvarnsvedens IK | 1.22 | 6.13 | 8.78 |
| 21:30 | 1307 | Gresford Athletic vs Guilsfield Athletic | 2.74 | 3.29 | 2.27 |
| 21:45 | 2319 | UCD Dublin vs Derry City | 11.65 | 5.56 | 1.18 |
| 21:45 | 4441 | Havant and Waterlooville vs Eastbourne Borough | 2.18 | 3.52 | 2.80 |
| 22:00 | 2379 | Real Soacha Cundinamarca vs Leones FC | 2.35 | 3.15 | 2.80 |
| 22:00 | 3996 | Tigres FC (COL) vs Bogota FC | 2.27 | 2.76 | 3.37 |
| 22:00 | 4772 | Municipal Turrialba vs Guadelupe FC | 3.05 | 3.40 | 2.01 |
| 22:00 | 5963 | Libya vs Equatorial Guinea | 3.17 | 3.06 | 2.28 |
| 23:00 | 2023 | Municipal Santa Ana vs CD Escorpiones Belen | 2.09 | 3.61 | 2.90 |
| 23:00 | 4445 | Limon Black Star vs Futbol Consultants Moravia | 1.62 | 3.87 | 4.48 |
| 23:30 | 2357 | 9 De Octubre FC vs Chacaritas FC | 1.77 | 3.36 | 4.18 |
| 23:30 | 2469 | Vargas Torres vs CD Alianza Cotopaxi | 2.69 | 2.69 | 2.80 |
| 23:30 | 5885 | Quepos Cambute vs ADR Jicaral | 3.10 | 3.36 | 2.08 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SIMBA YAJA NA 'BACK TO SCHOOL' KUWAVUTA WATOTO MICHEZONI

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kuanza kusaka vipaji katika soka la vijana, wanawake na timu ya wakubwa kuwa miongoni mwa klabu kubwa barani Afrika, uongozi wa Klabu ya Simba umezindua programu maalum ya kuibua vipaji vya watoto mashuleni waliyoipa jina la 'Back to School'.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa Simba, Iman Kajula, alisema wameamua kurudi shuleni kwa makocha wa timu za vijana kuzitembelea shule siku za michezo ili kuwaweka karibu watoto na Simba.

**Alisema wanatambua katika shule kuna vipaji na wanaenda huko kuibua wachezaji wapya, lakini pia kuwaandaa mashabiki wa Simba wa baadaye kupitia programu hiyo.**

"Programu hiyo itakuwa endelevu kutembelea shule zote hapa nchini huku makocha wetu wa vijana wakifanya programu zao, lakini pia siku za mechi watoto katika shule mbalimbali watapewa nafasi ya kuja uwanjani kuisapoti timu yao," alisema Kajula.

Alisema Simba walizungumza na wabia wao (taasisi za mabenki) kuhakikisha wanakuwa na akaunti za watoto ili wanapofungua wanakuwa sehemu ya mashabiki.

"Wabia wetu wamekubali hilo na sasa mzazi anapokwenda kumfungulia mtoto akaunti anakuwa sehemu ya mwanachama wa Simba, tumeenda mashuleni kwa sababu elimu na michezo inawafanya watoto wetu kuwa na utimamu wa mwili (afya ya akili) na kujenga ushirikiano wenyewe kwa wenyewe na nidhamu," alisema Kajula.

Naye Meneja wa Programu za Vijana Simba, Patrick Rweyemamu, alisema baada ya kufanikiwa kupata timu za vijana kuanzia umri chini ya miaka (U-17) na (U-20), sasa wanaenda katika shule za msingi na kindagate kwa ajili ya kuibua vipaji vya watoto.

Alisema miaka ya sasa watoto wamepoteza hamu ya kucheza mpira wa miguu kwa sababu ya changamoto za viwanja kuwa duni, sasa Simba wameamua kurudisha mapenzi ya kupenda kucheza na kuibua vipaji.

"Hii haitakuwa faida kwa Simba pekee bali ni kwa Taifa letu, tunapotengeneza programu hii inasaidia kuibua vipaji kuanzia chini na baadaye itakuwa rahisi kupata wachezaji wazuri na kuleta manufaa kwa timu zetu za taifa za kike na kiume," alisema Rweyemamu.




Katibu wa Mbunge wa Jimbo la Geita Mjini, Mariam Mkaka (kulia), akimkabidhi jezi Mwenyekiti wa timu ya VEN FC, Agata Elias, ambaye ni miongoni mwa viongozi wa timu 14 jimboni hapo zinazoshiriki Ligi Daraja la Nne Wilaya ya Geita, waliokabidhiwa jezi, mipira 16 pamoja na vifaa vingine vya michezo juzi, vyenye thamani ya Sh. milioni 6.6. **PICHA: ALPHONCE KABILONDO**

## Gamondi afunguka...

INATOKA UKURASA 24

wanacheza vipi na hata ugenini, " alisema Gamondi.

Aliongeza kuwa kwa siku chache alizokuwapo hapa Tanzania, ameona wachezaji wengi wenye vipaji ndani ya timu yake na kuwapa nafasi ndani ya kikosi chake.

"Ni kweli Tanzania ina vipaji, hivi karibuni nilikuwapo Zanzibar nimeona wachezaji wenye kiwango kizuri, matarajio yangu msimu ujao nitakuwa sehemu ya 'skauti' ili kupata wachezaji wazuri na wazawa ambao wataisaidia timu," alisema kocha huyo.

Kwa upande wa Afisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, alisema timu imeingia kambini kwa ajili ya maandalizi ya mechi yao dhidi ya Al-Merrikh na wanatarajia kucheza mechi moja ya kirafiki kabla kwenda Rwanda Septemba 14 na 15 tayari kwa mechi hiyo.

## *Miquissone aahidiwa...*

INATOKA UKURASA 24

kila hatua tunayopiga huwa tunaimarika, angalia mechi ya robo fainali iliyopita dhidi ya Wydad Casablaca, tulitolewa lakini ilikuwa kwa penalti, haikuwa kama zile za nyuma tulizokuwa tunatolewa," alisema.

Naye kiungo mkabaji mpya wa timu hiyo, Hamisi Abdallah, alisema wachezaji wapya wa timu hiyo wamefurahia kucheza mechi hiyo kubwa kwa sababu ni nafasi yao ya kujitangaza.

"Sisi kama wachezaji tuliojiunga na Simba ni mechi kubwa sana kwetu na tulikuwa tunahitaji kucheza na timu kubwa kwenye viwanja vikubwa ili kuonekana, kuonesha tulichonacho na kujitangaza, nadhani dakika 90 za nyumbani na ugenini zitaamua, ila sisi tumejipanga vema," alisema.

Wakati huohuo jana asubuhi, katika Uwanja wa Mo Arena, Bunju, Dar es Salaam, kikosi cha timu hiyo kilicheza mechi ya kirafiki dhidi ya Cosmopolitan FC ambayo inajiandaa na Ligi ya Championship na kushinda mabao 5-1.

Mabao ya Simba yalifungwa na Moses Phiri, Jean Baleke, Willy Onana, Aubin Kramo na Shaaban Chilunda.

Michezo
Jumatano Septemba 6, 2023
Nipashe



‘Mimi na Messi tumeishi kama kuzimu’ UKURASA 21

# Miquissone aahidiwa ushindi Simba, Al Ahly

●●● Kupambana hadi tone la mwisho huku Phiri, Baleke, Onana, Kramo wakifanya...



Luis Miquissone akimiliki mpira dhidi ya Fabrice Ngoma mazoezini juzi. **PICHA: SIMBA**

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI wakiendelea kujiandaa kwa ratiba ngumu ya michuano miwili tofauti ya kimataifa iliyopo mbele yao; Ligi ya Mabingwa Afrika na African Football League (AFL), wachezaji wa Simba wametoa ahadi nzito kwa nyota mwenzao, Luis Miquissone.

**Ratiba inayofuata kwa Simba ni mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos ya Zambia Septemba 16, ugenini na kisha timu hizo kurudiana jijini Dar es Salaam Septemba 29, mwaka huu.**

Baada ya hapo Oktoba 20, mwaka huu, itakuwa na kibarua kigumu dhidi ya Mabingwa Watetezi wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Al Ahly, katika mchezo wa ufunguzi wa African Football League utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mechi hiyo imekuwa ikimulikwa zaidi kuanzia kwa mashabiki wa Simba, viongozi, benchi la ufundi hadi wachezaji, na sasa nyota wa kikosi hicho wametoa ahadi kwa mchezaji mwenzao, Miquissone kwamba watacheza kwa nguvu zote hadi tone la mwisho la jasho ili kupata ushindi wa mabao mengi katika mechi yao dhidi ya Al Ahly kwa ajili ya kumpa zawadi winga huyo aliyetoka kwenye kikosi cha wababe hao wa Misri na kurejea Msimbazi.

Beki wa kulia wa timu hiyo, Shomari Kapombe amesema wachezaji wote wa timu hiyo wamekaa na kuambizana kuwa ni lazima wacheze kwa juhudi kubwa dhidi ya timu hiyo kubwa na Mabingwa wa Afrika kwa ajili ya mwenzao ambaye amesema atajisikia raha sana kama watashinda mchezo huo.

Akizungumza juzi jioni jijini Dar es Salaam, Kapombe amekiri kuwa mechi ya African Football League itakuwa ngumu, lakini safari hii wamejipanga si tu kushinda katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, bali kuing’oa Al Ahly mashindanoni kwa mara ya kwanza.

“Ni bahati kubwa kuweza kupata kucheza tena na Al Ahly, pia kuwamo kwenye mashidano haya mapya na kuwa moja kati ya klabu kubwa mpya nane zilizochaguliwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), sisi kama Klabu ya Simba inabidi tujivunie, tunakwenda kucheza mechi hii huku Miquissone akiwa amerejea kwenye kikosi chetu kutoka kwao.

“Ni changamoto nzuri kwetu kwa sababu tunacheza kwa ajili ya kitu fulani, na yeye itakuwa ni chachu kwake na sisi tumekaa kikao kama wachezaji, tumeahidi kumpa sapoti kubwa tuweze kumpa zawadi ya ushindi, pamoja na kwamba wanachama na mashabiki na sisi wachezaji tutafurahi, lakini na yeye ajisikie vizuri zaidi,” alisema Kapombe.

Alisema kuwa mechi itakuwa bora kwa sababu zitacheza timu kubwa zenye viwango vya juu Afrika, lakini pia kutokana na michezo iliyopita rekodi iliyopita Uwanja wa Benjamin Mkapa kwani kila wanapokutana nao wanaondoka na ushindi.

“Kila tunapokutana nao tumewafunga mara zote, sisi wengine tulikuwapo, lakini huu ni mchezo mwingine, safari hii kuna baadhi ya sura zingine, baadhi ya wachezaji wengine na nafasi nyingine,” alisema.

Kapombe aliwahakikishia mashabiki wa Simba kuwa safari hii wanataka kufanya vema kwenye mechi zote mbili ikiwamo ile ya marudiano itakayochezwa nchini Misri Oktoba 24.

“Sisi kwa Mkapa tutaendelea na rekodi yetu, tulipoishia tutaendelea pale pale, na mashabiki wa Simba wasiwe na wasiwasi mechi ya marudiano, ukiangalia Simba

INAENDELEA UKURASA 23

# Gamondi afunguka kuisoma Al-Merrikh

**Na Saada Akida**

HUKU Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, akisema bado kikosi chake hakijafikia asilimia 100 ya namna anavyotaka kiwe, pia amefunguka kwamba tayari amewaona wapinzani wao Al-Merrikh namna wanavyocheza na wachezaji wao wakuchungwa.

Yanga imeingia kambini jana tayari kwa ajili ya mchezo wao wa raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al- Merrikh utakaopigwa nchini Rwanda Septemba 16, mwaka huu, kutokana na Sudan wanapotoka wapinzani wao hao kuwa na machafuko ya kisiasa.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema licha ya kuendelea kufanya vizuri katika michuano wanayoshiriki, lakini bado hajafikia asilimia 100 kwa wachezaji wake kufanya anachokitaka ili kuweza kufikia malengo ya klabu msimu huu.

Alisema licha ya changamoto hiyo, anaamini ndani ya muda mchache anaweza kupata anachokitaka kutoka kwa wachezaji wake.

“Tumebakiwa na wachezaji wachache kutokana na wengi kuwa katika majukumu ya timu za taifa kabla ya kurejea na kuendelea na mikakati yetu, tumekuwa tukifanya mazoezi ufukweni kwa ajili ya kujenga stamina kwa wachezaji pamoja na kubadilisha mazingira kwa sababu tunajipanga kulingana na ubora wa wapinza wetu kwenye Ligi ya Mabingwa

“Tumefanikiwa kuona ubora wao na wachezaji gani wakuwachunga, wanapokuwa nyumbani

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002